

**UCHANGANUZI WA KIPRAGMATIKI WA UTOUPOLE KATIKA
FILAMU ZA KISWAHILI**

LILIAN CHACHA NYANGI

**Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya
shahada ya uzamili katika masomo ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.**

2017

UNGAMO

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo chochote kwa minajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili.

Lilian Chacha Nyangi

C50/ 80486 / 2015

Sahihi..... Tarehe.....

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

PROF. JOHN HABWE

Sahihi..... Tarehe.....

PROF. IRIBE MWANGI

Sahihi..... Tarehe.....

TABARUKU

Kwa wazazi wangu wapendwa:

Baba yangu Joseph Chacha na mama yangu Immaculate Chacha.

SHUKRANI

Ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu Prof. John Habwe na Prof. Iribe Mwangi kwa mawaidha yao ya busara na kwa kusoma kazi hii na kunikosoa na kunipa mwelekeo unaofaa. Shukrani sana na Mungu awabariki. Nawashukuru pia wahadhiri wote katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Idara ya Kiswahili kwa mafunzo na ushauri wenu mwema. Shukrani zangu ziwafikie Prof. Abdulaziz, Prof. Rayya Timammy, Dkt. Zaja, Prof. Kineene, Dkt. Mukhwana, Dkt. Swaleh, Dkt. Mbuthia, Dkt. Buregeya, Dkt. Olali, Dkt. Mwaliwa na Dkt. Jerono.

Shukrani zingine ziwafikie wanafunzi wenzangu tuliosoma pamoja. Hawa ni Kolongei Purity, Kitiku Zipporah, Ngulamu Mwaviro, Otvera Albert, Anusu Joshua, Muna Edwin na Samuel Ngunyi. Mwisho siwezi kuwasahau wale ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia kufanikisha utafiti huu. Kwenu nyote nasema shukrani.

IKSIRI

Tasnifu hii imeshughulikia suala la utoupole katika filamu nne za Kiswahili kutoka Tanzania ambazo ni *Hila*, *Tabasamu Ghushi*, *Upepo wa baridi* na *Majuto* ambazo ziliteuliwa kimakusudi ili kutupatia data iliyoweza kufanikisha malengo ya utafiti huu. Data ya utafiti huu ilitokana na uchambuzi wa kauli za waigizaji wa filamu husika na kuzichanganua kwa msingi wa nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996). Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kubainisha na kujadili mikakati ya utoupole katika kauli za waigizaji wa filamu husika. Matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba mikakati ya utoupole iliyopendekezwa na Culpeper (1996) inatumiwa na waigizaji wa filamu husika kwa lengo la kuhasiri nyuso za waigizaji wenzao. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kwamba mkakati ndani ya rekodi wa utoupole ndio mkakati unaotumiwa zaidi na waigizaji wa filamu husika huku ukirekodi frikwensi ya asilimia 45.2 %, huku mkakati wa kutowasilisha chochote ukiwa mkakati ambao hautumiwi sana kwa kurekodi frikwensi ya asilimia 4.0%. Vilevile, uchunguzi huu ulilenga kuchunguza namna waigizaji wa filamu husika wanakabiliana na hali ya utoupole katika mazungumzo. Matokeo yamebainisha kwamba mbinu ya msikilizaji kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso ndiyo mbinu inayotumiwa zaidi huku ikirekodi frikwensi ya asilimia 60 %.

MAELEZO YA ISTILAHU MUHIMU KAMA ZILIVYOTUMIKA KATIKA UTAFITI

Upole – Matumizi ya lugha ya mazungumzo yanayodhihirisha heshima.

Utoupole – Matumizi ya lugha ya mazungumzo yanayodhihirisha utovu wa adabu na heshima.

Mikakati ya utoupole - Mbinu mbalimbali zinazotumiwa na waigizaji wanapozungumza ili kuvunja mazungumzo kati yao.

Vitendo vinavyohasiri uso – Kauli ambazo hukasirisha msikilizaji au msemaji wakati wa mazungumzo na kupelekea kuvunjika kwa mazungumzo.

Mchakato – Mfululizo wa shughuli unaosababisha kitu fulani kufanyika au lengo fulani kufikiwa.

YALIYOMO

UNGAMO	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI	iv
IKSIRI	v
MAELEZO YA ISTILAHU MUHIMU KAMA ZILIVYOTUMIKA KATIKA UTAFITI	vi
ORODHA YA MICHORO	xi
SURA YA KWANZA: MSINGI WA UTAFITI	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Tatizo la Utafiti	3
1.3 Malengo ya Utafiti.....	3
1.4 Nadharia Tete	4
1.5 Umuhimu wa Utafiti.....	4
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti	4
1.7 Msingi wa Nadharia ya Utafiti	5
1.7.1 Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987).....	5
1.8 Nadharia ya Utoupole ya Jonathan Culpeper (1996)	8
1.8.2 Mkakati Chanya wa Utoupole	9
1.8.3 Mkakati Hasi wa Utoupole.....	9
1.8.4 Matumizi ya Kejeli.....	10
1.8.5 Kutowasilisha Chochote.....	10
1.9 Yaliyoandikwa.....	11
1.9.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ya Utafiti	11
1.9.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Filamu za Kitanzania.....	17
1.10 Mbinu za Utafiti	19

1.10.1 Mbinu za Kukusanya Data	19
1.10.2 Uteuzi wa Sampuli	19
1.10.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data	20
1.11 Muhtasari wa Sura.....	21
SURA YA PILI: UPOLE NA UTOUPOLE KATIKA MAWASILIANO	22
2.1 Utangulizi	22
2.2 Upole	22
2.3 Utaratibu wa Ushirikiano (Grice 1975).....	23
2.4 Upole kama Mkataba wa Mazungumzo (Fraser na Nolen 1981).....	24
2.5 Kanuni za Upole za Leech (1983)	25
2.6 Upole kama Mkakati wa Kuokoa Uso	27
2.7 Utoupole katika Mawasiliano.....	27
2.8 Dhana ya Utoupole na Arudhi.....	29
2.8.1 Dhana ya Kiimbo na Utoupole	30
2.9 Hali Zinazoathiri Matumizi ya Mikakati ya Utoupole katika Mawasiliano.....	32
2.9.1 Tofauti za Kimamlaka kati ya Msemaji na Msikilizaji	32
2.9.2 Utoupole na Mahusiano ya Kijamii.....	34
2.10 Hitimisho	35
SURA YA TATU: MATUMIZI YA MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA FILAMU ZA KISWAHILI.....	36
3.1 Utangulizi	36
3.2 Sinopsia ya Filamu ya <i>Upepo wa Baridi</i>	36
3.3 Sinopsia ya Filamu ya <i>Hila</i>	37
3.4 Sinopsia ya Filamu ya <i>Majuto</i>	38
3.5 Sinopsia ya Filamu ya <i>Tabasamu Ghushi</i>	39

3.6 Matumizi ya Mkakati Ndani ya Rekodi wa Utoupole.....	40
3.7 Matumizi ya Mkakati Chanya wa Utoupole.....	43
3.7.1 Matumizi ya Lugha ya Matusi.....	43
3.7.2 Msemaji Kutotaka Kujihusisha na Msikilizaji	46
3.7.3 Msemaji Kumpa Msikilizaji Utambulisho Usiofaa.....	47
3.8 Matumizi ya Mkakati Hasi wa Utoupole	49
3.8.1 Matumizi ya Kebehi	49
3.8.2 Msemaji Kumhusisha Msikilizaji na Uhasi.....	50
3.8.3. Msemaji Kuingilia Faragha ya Msikilizaji.....	51
3.9 Matumizi ya Kejeli.....	53
3.10 Kutowasilisha Chochote.....	54
3.10.1 Kutojibu Salamu.....	54
3.10.2 Kutoshukuru	55
3.6 Hitimisho	58
SURA YA NNE: NAMNA YA KUKABILIANA NA HALI YA UTOUPOLE	59
4.1 Utangulizi	59
4.2 Kukubali Vitendo Vinavyohasiri Uso	59
4.3 Kukabili Vitendo Vinavyohasiri Uso.....	60
4.3.1 Kukabili Vitendo Vinavyohasiri Uso kwa Namna ya Kujikinga	60
4.3.2 Kukabili Vitendo Vinavyohasiri Uso kwa Namna ya Kumshambulia Msemaji.....	61
4.4 Kuwa Kimya.....	63
4.5 Hitimisho	67
SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	68
5.1 Utangulizi	68
5.2 Kutathmini Ufanisi wa Malengo ya Utafiti	68

5.3 Changamoto za Utafiti.....	69
5.4 Mapendekezo.....	70
MAREJELEO.....	71
VIAMBATISHO.....	74
Kiambatisho I	74
Kiambatisho II.....	81
Kiambatisho III	87
Kiambatisho IV.....	93

ORODHA YA MICHORO

Jedwali 1: Frikwensi ya Matumizi ya Mikakati ya Utoupole katika Filamu Husika.....	57
Jedwali 2: Frikwensi ya Matumizi ya Mbinu za Kukabiliana na Utoupole Katika Filamu Husika.....	65

SURA YA KWANZA

MSINGI WA UTAFITI

1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulilenga kujadili suala la utoupole katika filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Wasanii wa filamu wanatumia sanaa hii kama njia mojawapo ya kuelimisha jamii, kuonya, kuasa, kukosoa, kuadilisha, kutunza amali za jamii na kuelekeza hisia na matamano yao kwa jamii husika. Wasanii wa filamu hizi hutumia lugha kuwafahamisha watazamaji kuhusu masuala tofauti ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Wasanii maarufu kwenye tansia ya filamu nchini Tanzania ni pamoja na marehemu Steven Kanumba, Vincent Kigosi, Patcho Mwamba, Mahsein Awadhi, Elizabeth Michael, Riyama Ali, Aunty Ezekiel, Jennifer Mgendi na wengine.

Ili kufanikisha mawasilino, watu hutumia lugha ya upole ili kuepuka kuwaudhi wasikilizaji wao. Leech (1983) anasema kwamba dhana ya upole ni tabia ambayo huwawezesha washiriki katika mazungumzo kuhusika katika mtagusano wa kijamii katika hali ya uwiano na kiupatano. Leech anafafanua kuwa, jambo muhimu zaidi katika mawasiliano ni kudumisha mazingira ambayo yatadumisha mawasiliano. Aidha, Brown na Levinson (1987) wanadai kwamba katika mazungumzo kuna vitendo ambavyo vinaweza kutishia nyuso za msemaji na msikilizaji. Vitendo hivyo ni kama vile: Kuamrisha, kutoa maagizo, kuonya, kutoa ushauri kwa msikilizaji n.k. Culpeper (1996) kwa upande mwingine anadai kwamba kuna vitendo ambavyo vinaweza kuhasiri uso wa msikilizaji ambavyo ni pamoja na: kutusi, kukashifu, matumizi ya lugha ya vitisho, matumizi ya mada za miiko hasa zilizokatazwa na utamaduni wa msikilizaji, urejeleaji wa msikilizaji kwa namna hasi, na kumdunisha msikilizaji kihadhi miongoni mwa vitendo vingine.

Brown na Levinson wanapendekeza mikakati minne ya upole ambayo hutumiwa katika mazungumzo ili kuepuka kuhasiri uso wakati wa kutenda vitendo vinavyotishia uso ambayo ni: Mkakati ndani ya rekodi, mkakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole na mkakati nje ya rekodi. Mikakati hii hulenga kuhifadhi nyuso za msemaji na msikilizaji. Naye Culpeper anapendekeza mikakati mitano ya utoupole ambayo hutumiwa kimakusudi na wasemaji katika mazungumzo ili kuhasiri nyuso za wasikilizaji wao.

Culpeper (1996) anadai kuwa matumizi ya mikakati ya upole na mikakati ya utoupole katika mawasiliano hutegemea lengo la msemaji katika mchakato mzima wa mawasiliano. Anaeleza kuwa, msemaji anaweza kutumia mikakati ya upole katika mazungumzo kwa lengo la kuhifadhi uso wa msikilizaji lakini wakati mwingine msemaji huwa na nia ya kuhasiri uso wa msikilizaji kimakusudi kwa kutenda vitendo vinavyodhuru uso wa msikilizaji. Zaidi ya hayo, hali hii inaweza kusababisha mgongano wa kijamii.

Hali hii haidhihiriki tu kwenye ulimwengu wa kiuhalisia bali pia kwenye kazi andishi na simulizi za kifasihi hasa kwenye filamu. Kwa msingi huu, utafiti huu ulichunguza suala la utoupole katika filamu nne za Kiswaliili. Utafiti huu ulichunguza kauli za waigizaji wa filamu husika zinazosawiri mikakati ya utoupole na kuifafanua mikakati hiyo kwa msingi wa nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996).

1.2 Tatizo la Utafiti

Watafiti wengi wametafitia kuhusu suala la upole na umuhimu wake katika kuanzisha na kudumisha mahusiano katika jamii, hasa tafiti zao zikiendelezwa na nadharia ya uso ya upole ya Brown na Levinson (1987). Kwa upande mwingine, suala la utoupole katika mazungumzo na namna linavyopelekea kuvunjika kwa mazungumzo na kusababisha migongano ya kijamii halijatafitiwa kwa kina. Ni tafiti chache sana ambazo zimegusia suala la utoupole katika mazungumzo hasa tafiti hizi zikijikita katika filamu za nchi za ulaya. Hata hivyo, kwa ufahamu wangu hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusu suala la utoupole katika filamu za Kiswahili. Ni kutokana na kuwepo kwa pengo hili la kutokuwepo na utafiti ambao umefanywa katika filamu za Kiswahili kwa kuchunguza suala la utoupole ambapo utafiti huu unapata msingi wake.

1.3 Malengo ya Utafiti

Lengo maalum la utafiti huu lilikuwa kuchunguza suala la utoupole kwenye filamu nne za Kiswahili ambazo ni: *Hila*, *Tabasamu Ghushi*, *Upepo wa Baridi na Majuto*. Malengo mahsusi ya utafiti huu ni:

1. Kubainisha na kijadili mikakati ya utoupole katika kauli za waigizaji wa filamu husika.
2. Kujadili namna waigizaji wa filamu husika wanavyokabiliana na hali ya utoupole katika mazungumzo.

1.4 Nadharia Tete

1. Suala la utoupole ni dhahiri katika mazungumzo ya waigizaji wa filamu hizi za Kiswahili.
2. Waigizaji wa filamu hizi hukabiliana na hali ya utoupole kwa namna ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso.

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Suala la utoupole halijafanyiwa utafiti kwa kina. Hivyo basi kila nyongeza katika dhana hii ni mchango muhimu katika uendelezaji wa dhana hii. Uchunguzi huu utafungua ukurasa wa tafiti nyingine kuhusu suala la utoupole katika kuchambua diskosi na kauli mbalimbali katika kazi za fasihi ya Kiswahili zikiwemo riwaya, hadithi fupi, tamthilia na novela. Hali kadhalika, utafiti huu utawafaa watafiti wengine na wanajamii kwa jumla katika kubainisha jinsi wanajamii mbalimbali hutumia mikakati ya utoupole katika mazungumzo kama tukio la kimakusudi kwa lengo la kusababisha migongano ya kijamii.

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unakita katika mtagusano wa Semantiki na Pragmatiki hasa jinsi dhana ya utoupole inavyoingizwa katika mazungumzo ya waigizaji wa filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Hivyo basi, utafiti huu unahusisha filamu za Kiswahili kutoka nchini Tanzania na wala si nchi nyingine ile. Utafiti huu ulichunguza filamu nne pekee ambazo zimetungwa na kuongozwa na wasanii tofauti ambazo ni: *Tabasamu Ghushi*, *Upepo wa Baridi*, *Pigo Majuto* na *Hila*. Masuala muhimu kwenye filamu hizi ni pamoja na athari za matumizi ya dawa za kulevya, malezi, umaskini, changamoto mbalimbali kwenye asasi ya ndoa, usaliti kwenye mapenzi miongoni mwa mengine.

Kwa kutumia data ya mazungumzo katika filamu hizi, utafiti huu ulilenga kabainisha mikakati ya utoupole inayotumika katika mazungumzo ya waigizaji wa filamu husika. Hivyo basi mtafiti alijikita tu kwenye kauli za waigizaji pekee na wala si masuala mengine ya filamu kama vile miondoko na miswada andishi ya filamu husika. Utafiti huu uliendelezwa kwa kutumia nadharia ya utoupole iliyoasisiwa na Culpeper (1996) kwa kubainisha mikakati ya utoupole inayotumika katika filamu husika.

1.7 Msingi wa Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliendelezwa na nadharia ya utoupole iliyoasisiwa na Culpeper (1996). Culpeper (1996) alijenga nadharia ya utoupoleole kutokana na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) ambao walitumia dhana ya uso inayofungamanishwa na mwanasosholojia Goffman (1967) kubuni nadharia ya upole.

1.7.1 Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987)

Kwa mujibu wa Goffman (1967) uso ni thamani chanya ya kijamii ambayo mtu hujipa kulingana na mtazamo ambao watu wengine huchukulia kuwa ameegemea katika mtagusano fulani. Uso ni dhana bia na ni sura kibinafsi inayohusishwa na sifa za kijamii. Goffman (1967) anaeleza kwamba, mtu anapotunza uso wake humfanya ahisi vizuri kwa sababu anakuwa na uhusiano wa kihisia na uso ambao anautunza. Aidha, kupoteza uso husababisha kupotea kwa mhimili wa kihisia ambao huhifadhiwa katika hali za kijamii. Ili kuepuka kupoteza uso, watu wanapozungumza hujaribu kushiiriki katika vitendo vya kuokoa nyuso zao na za wasikilizaji wao. Brown na Levinson (1987) wanadai kwamba, uso ni sura ya mtu binafsi ya kijamii ambayo mtu huichukulia kuwa yake. Kwa mtazamo wa watalaamu hawa wa isimu, kila binadamu ana nyuso mbili ambazo ni uso chanya na uso hasi.

1.7.2 Uso Chanya na Uso Hasi

Uso chanya na uso hasi huelezwa kwa msingi wa matanianio ambayo kila binadamu huwa nayo na hufanya jitihada kuhakikisha kwamba yanathaminiwa. Nyuso hizi hudhihirisha matanianio mawili tofauti katika kila aina ya maingiliano. Uso hasi hutamani kuthaminiwa na kukubalika jinsi ulivyo bila kuhasiwa, kuwa na uhuru wa kutenda anavyotaka binadamu, kutoshuriwa na kutolazimishwa na wengine. Kwa upande mwingine, uso chanya hutamani mchango wake kukubaliwa, kushirikisliwa, huhitaji kusifiwa na kuthaminiwa na wengine kwa kutambuliwa kama sehemu ya kundi la jamii.

Kila wakati binadamu hutaka nyuso hizi mbili zihifadhiwe lakini wakati mwingine tendo la usemi la msemaji linaenda kinyume na matamaniao ya uso wa msikilizaji na kunatokea vitendo vinavyotishia kudhuru nyuso za msemaji na msikilizaji. Hivyo basi, uso lazima uzingatiwe katika mazungumzo kwa kuwa ni kitu dhaifu. Katika mawasiliano, uso unaweza ukahasiwa au kuumbuliwa, ukadumishwa au kujengwa. Hivyo basi ni muhimu katika mawasiliano msemaji kudumisha sio tu uso wake bali pia uso wa msikilizaji. Kwa msingi huu, msemaji lazima awe katika nafasi ya kuokoa au kuujenga uso wakati ambapo anakabiliwa na hali zinazotishia kuhasiri uso wa msikilizaji kama; amrishi, kukosolewa, kuaibishwa, kutokubaliwa miongoni mwa hali nyingine.

Brown na Levinson wanapendekeza mikakati minne ambayo msemaji anaweza kuitumia ili kukabiliana na hali zinazoweza kuhasiri uso. Mikakati hiyo ni: Mkakati ndani ya rekodi, mkakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole na mkakati nje ya rekodi. Mkakati ndani ya rekodi ni mkakati ambao haulengi kuonyesha upole wowote bali huwa ni kauli za moja kwa moja kama vile: Nataka hela. Mkakati huu hutumika sana pale ambapo mzungumzaji na msikilizaji wana uhusiano wa karibu ama wakati wa dharura na kuna haja ya kutoa msaada.

Mkakati chanya kwa upande mwingine hutambua uso wa msikilizaji na huepuka kuuhasiri na hudhihirisha urafiki au upamoja baina ya msikilizaji na msemaji: Mfano; Je, utajali kunisaidia na shilingi mia tano? Mkakati hasi huu kwa upande wake hutambua uso wa msikilizaji lakini wakati uo huo huonyesha kuwa unamshinikiza kufanya jambo fulani ila ulazimishaji umefichika. Kwa mfano; Sitaki kukusumbua sana lakini je, ninaweza nikapata kikombe cha chai? Nao mkakati nje ya rekodi hudhamiria kuondoa kuhasiwa kwa uso wa msikilizaji kwa kujaribu kuepuka kusema jambo moja kwa moja lakini wakati uo huo kuongea kwa namna inayomwelekeza msikilizaji kuwa anatakiwa afanye jambo fulani. Kwa mfano, badala ya kuitisha kikombe cha chai, msemaji anaweza akasema kauli kama hii: Kuna baridi sana, hali kama hii humfanya mtu ahisi kunywa chai.

Brown na Levinson wanaeleza kuwa suala la nyuso mbili katika maisha ya binadamu ni muhimu sana na hujidhihirisha kwa binadamu wote duniani. Kulingana na Brown na Levinson (1987) mikakati ya upole hubuniwa ili kuepuka kudhuru nyuso za msemaji na msikilizaji. Wanaueleza uso kama heshima ambayo mtu binafsi huwa nayo na ambayo hutarajia kudumishwa na wengine katika mikitadha ya umma na ya kibinafsi. Lakini kwa upande mwingine, Culpeper (1996) anadai kwamba siyo kila wakati katika mazungumzo msemaji hutumia mikakati ya upole kwa lengo la kuhifadhi nyuso za msikilizaji bali wakati mwingine katika mazungumzo, msemaji huwa na nia ya kudhuru uso wa msikilizaji kwa kutenda vitendo vinavyohasiri uso wa msikilizaji kimakusudi.

1.8 Nadharia ya Utoupole ya Jonathan Culpeper (1996)

Culpeper (1996) anadai kwamba utoupole hutokea katika hali ambapo msemaji hutenda kimakusudi vitendo vinavyohasiri uso wa msikilizaji na hivyo basi kusababisha kutoelewana kati yao, hali ambayo hupelekea kutokea mgongano wa kijamii. Culpeper (2001) anazidi kueleza kwamba tofauti ya msingi kati ya dhana ya upole na utoupole ni lengo la msemaji. Anasema kwamba, katika mchakato mzima wa mawasiliano, msemaji anapokusudia kuhifadhi uso wa msikilizaji basi huwa anazingatia suala la upole katika mawasiliano ilhali msemaji anaponuia kuhasiri uso wa msikilizaji, basi huwa anavuruga upole katika mawasiliano.

Culpeper (2005) anafafanua dhana ya utoupole kwa kina kwa kuhusisha jukumu la msikilizaji. Anaeleza kwamba utoupole hutokea wakati ambapo msemaji anatenda kimakusudi vitendo vinavyohasiri uso wa msikilizaji au wakati ambapo msikilizaji anatambua kwamba kitendo cha msemaji kinanua kudhuru uso wake au hali zote mbili. Kutokana nafafanuzi hizi kuhusu dhana ya utoupole, ni dhahiri kwamba utoupole unahusisha vitendo vinavyohasiri uso vinavyofanywa kimakusudi na msemaji kwa lengo la kudhuru uso wa msikilizaji ili kusababisha ugomvi au mgongano wa kijamii. Culpeper (1996) anapambanua mikakati mitano ya utoupole ambayo ni pamoja na: Mkakati ndani ya rekodi, mkakati chanya wa utoupole, Makati hasi wa utoupole, matumizi ya kejeli na kutowasilisha chochote.

1.8.1 Mkakati Ndani ya Rekodi wa Utoupole

Culpeper (1996) anaeleza kuwa, mkakati ndani ya rekodi hutumiwa katika hali ambapo msemaji ananua kudhuru uso wa msikilizaji na hivyo basi kauli ya msemaji kwa msikilizaji huwa dhahiri, yenye maneno machache lakini yenye habari nyingi au nzito kwa msikilizaji. Hali hii inadhihirika kwenye mazungu haya kati ya mume na mke katika mfano huu:

1. Mume : Miaka mingi imepita na hatujafanikiwa kupala mtoto wa kiume, niruhusu mke wangu, nijaribu karata nyingine.

Mke: Ati karata nyingine! Maanake mie nimekuwa karata nbovu sana, sio? Huoni haya? Mawazo yako haya ni ya kipumbavu.

Katika mazungumzo haya, mke anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa matumizi ya lugha ya matusi katika mazungumzo kudhuru uso chanya wa mume kwa kusema kwamba mumewe hana haya na mawazo yake ya kumwoa mke wa pili ni ya kipumbavu.

1.8.2 Mkakati Chanya wa Utoupole

Mkakati chanya wa utoupole hutumiwa kwa lengo la kudhuru mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji hasa matamano ya uso chanya wa msikilizaji ya kutaka kukubalika katika jamii. Mbinu ambazo hutumiwa kwenye mkakati huu ni pamoja na: Msemaji kumpuuza, beza au dharau msikilizaji, msemaji kutumia maneno ya miiko kwenye mazungumzo, msemaji kutotaka kujihusisha na msikilizaji na msemaji kumtusi msikilizaji.

1.8.3 Mkakati Hasi wa Utoupole

Mkakati hasi wa utoupole hutumiwa kwa lengo la kudhuru uso hasi wa msikilizaji. Mbinu zinazotumiwa kwenye mkakati huu ni pamoja na: msemaji kuingilia faragha ya msikilizaji, msikilizaji kumdhalilisha msemaji kwa maneno ya kebehi na msemaji kumrejelea msikilizaji kwa namna hasi.

1.8.4 Matumizi ya Kejeli

Matumizi ya kejeli katika mazungumzo ni mkakati ambao huhusisha msemaji kuonekana kuwa mpole kwa msikilizaji ilhali katika bali halisi, msemaji huwa hajakusudia kuonyesha upole wowote kwa msikilizaji. Mbinu inayotumiwa katika mkakati huu inahusisha msemaji kutumia implikecha kwa lengo la kuwasilisha ujumbe kinyume na alichokusudia kuwasilisha kwa msikilizaji. Kwa mfano, msemaji anapomwambia msikilizaji kwamba awe na siku njema katika hali ambapo wamekuwa na ugomvi mkali, ni dhahiri kwamba, hisia za ndani za msemaji si halisi.

Mkakati huu pia hutekelezwa kwa kutumia vitendo vinavyotishia uso kwa kutumia mikakati ya upole ambapo msemaji huwa hajadhamiria kuonyesha upole kwa msemaji. Mbinu mojawapo ya kutekeleza mkakati huu ni pale ambapo msikilizaji anapoulizwa swali linalohitaji jibu la la au ndio, badala yake msemaji anajibu kwa kejeli.

1.8.5 Kutowasilisha Chochote

Mkakati wa kutowasilisha chochote ni mkakati ambao unahusu kuwa kimya wakati ambapo upole unatarajiwa. Mbinu mojawapo ya mkakati huu ni kutosema asante katika hali ambapo ni desturi, kawaida, mazoea au ada ya kusema asante na vilevile kutojibu salamu wakati wa mamkizi.

Ni bayana kwamba Culpeper (1996) anatambua mikakati mitano ya utoupole ambyo ni: mkakati ndani ya rekodi, mkakati chanya, mkakati hasi, matumizi ya kejeli na kutowasilisha chochote. Kimsingi, nadharia ya utoupole ni kimelea cha nadharia ya uso ya upole ya Brown na Lenvinson (1987).

1.9 Yaliyoandikwa

1.9.1 Yayoandikwa Kuhusu Nadharia ya Utafiti

Watalamu wengi wamefanikisha kuibuka, kukua na kuendelea kwa nadharia ya utoupele ya Culpeper (1996). Baadhi ya watalamu ambao wameiwekea msingi wa kimawazo nadharia hii ni Lachenict (1980) na Brown na Levinson (1987) ilhali wengine kama vile Eelen (2001) na Bousfield na Locher (2008) wameihakiki na kuindeleza nadharia hii. Culpeper ambaye aliasisi nadharia hii vilevile ameindeleza katika kazi zake za hivi karibuni. Katika sehemu hii, mtafiti anashughulikia mawazo ya wataalam hawa kuhusu mchango wao katika nadharia hii pia katika utafiti huu kwa jumla.

Lachenict (1980) alipambanua mikakati minne ya utoupole kwenye mazungumzo ambayo hulenga kukera msikilizaji. Mikakati hiyo ni pamoja na mkakati nje ya rekodi, mkakati ndani ya rekodi, mkakati chanya na mkakati hasi. Mkakati nje ya rekodi unahusisha matumizi ya lugha ya matusi na kejeli kwenye mazungumzo. Mkakati ndani ya rekodi huhusisha matumizi ya vitendo vinavyotishia uso na kukatiza au kuingilia mazungumzo ya wengine. Mkakati chanya huhusisha kutomtambua msikilizaji kama sehemu ya kundi fulani kwenye jamii. Mkakati hasi huhusisha kumlazimisha msikilizaji kutenda jambo fulani, kuingilia uhuru wa msikilizaji na kudhuru hadhi yake kwenye jamii. Mawazo ya Culpeper (1996) yanaelekea kufanana na mawazo ya Lachenict (1980) lakini tofauti ni kwamba, Culpeper amefafanua dhana ya utoupole kwa kina ikilinganishwa na Lachenict. Hata hivyo, mawazo ya Lachenict ni muhimu katika utafiti huu kwa vile yanaingiliana kwa kiasi fulani na mawazo ya Culpeper.

Mwanaisimu mwingine ambaye ameshughulikia suala la utoupole kinadharia ni Eelen (2001). Eelen ni mmoja wa wanaisimu wa kwanza kutafiti dhana ya uvurugaji wa upole na kuibua wazo kuwa utoupole katika mazungurnzo wakati mwingine ni suala ambalo ni vigurnu kuliepuka na ni suala ambalo linahitaji kutafitiwa. Eelen (2001) anaeleza hali ambayo inaweza kusababisha utoupole kwenye mawasiliano. Anadai kwamba utoupole unaweza kutokea katika hali ambapo watu hukosa kujibu salamu wanaposalimiwa na badala yake wanaona ni heri wawe kimya. Culpeper (2005) anatoa maoni sawa na Eelen anaposema kwamba, mtu anapokosa kushukuru anapopewa zawadi au kufanyiwa jambo fulani, hali hii hudhihirisha utoupole kwenye mawasiliano.

Bousfield na Locher (2008) ni wanaisimu wengine ambao wanaangazia dhana ya utoupole kwa kuegemea mkabala wa kipragimatiki. Bousfield na Locher wanafasiri dhana ya utoupole kama aina ya tabia ambayo hukusudia kudhuru uso wa mtu kwenye mchakato mzima wa mawasiliano. Wanadai kwamba, utoupole kwenye mazungumzo hulenga kukasirisha msikilizaji katika hali mahususi. Bousfield na Locher wanafafanua namna mbalimbali za kukabiliana na utoupole katika mazungumzo. Kulingana nao, utoupole kwenye mazungumzo wakati mwingine ni suala lisiloepukika. Msemaji anapofanya vitendo vinavyodhuru uso wa msikilizaji, kuna namna mbalimbali ambazo msikilizaji anaweza kukabiliana na hali hii.

Bousfield na Locher (2008) wanaeleza kwamba, msikilizaji anaweza kukubali vitendo vinavyodhuru uso au akakabiliana na hali hii au akakimya. Msikilizaji anapokabiliana na hali hii, anaweza kujikinga au akamshambulia msemaji. Msikilizaji hukubali vitendo vinavyodhuru uso wake kutoka kwa msemaji anapokubaliana na kauli za msemaji ambazo hunuia kudhihirisha utoupole katika mawasiliano.

Kwa upande mwingine, msikilizaji anapokabili hali hii kwa lengo la kujikinga dhidi ya vitendo vinavyodhuru uso anaweza kumjibu msemaji au kumwelezea jambo fulani kwa namna ambayo haidhuru uso wa msemaji. Msikilizaji anapokabiliana na hali hii kwa lengo la kumshambulia msemaji, huitikia kwa kutenda vitendo vinavyodhuru uso wa msemaji. Hali kadhalika, msikilizaji anapokuwa kimya wakati ambapo anakabiliwa na vitendo vinavyodhuru uso, huwa labda amekimya kimakusudi au msemaji hampi nafasi ya kuzungumza au huwa haelewi kauli za msemaji.

Bousfield na Locher wanakubaliana na mawazo ya Culpeper na wengine (2003) wanaodai kwamba, msikilizaji anapokumbwa na hali ya utoupole kwenye mawasiliano, anaweza akaikubali hali hii au akakabiliana na hali hii au hata kuwa kimya. Mawazo ya Bousfield na Locher ni muhimu katika utafiti huu kwa vile yanaiendeleza nadharia ya utoupole ya Culpeper hasa kwenye kipengele cha namna ya kukabiliana na utoupole kwenye mazungumzo. Mawazo yao yalisaidia kuchunguza namna ambavyo waigizaji wa filamu zilizoteuliwa kufanyiwa utafiti wanakabiliana na utoupole kwenye muzungumzo.

Vilevile, Bousfield na Locher (2008) wameendeleza nadharia ya utoupole kwa kujadili dhana ya mamlaka na utoupole. Wanadai kwamba, msikilizaji na msemaji wakati mwingine huwa wametenganishwa katika uhusino na mamlaka au uwezo fulani. Msemaji anapokuwa na mamlaka au nguvu zaidi ya msikilizaji, kauli za msemaji zinaweza kudhihirisha utoupole kwenye mazungumzo kati yao.

Bousfield na Locher wanakubaliana na mawazo ya Culpeper (1996) anayedai kwamba, utoupole kati ya msemaji na msikilizaji unaweza kutokea kwenye mazungumzo katika hali ambapo msemaji ana nguvu au mamlaka zaidi ya msikilizaji. Katika hali hii, msemaji anaweza kumnyima msikilizaji haki ya kuzungumza au hata akatumia lugha ya vitisho

msikilizaji anapokabiliana na hali hii kwa kumshambulia msemaji. Mawazo ya Bousfield na Locher kuhusu dhana ya mamlaka na utoupole ni muhimu katika utafiti huu kwa vile yanagusia suala la mamlaka na utoupole ambayo pia utafiti huu unaangizia.

Culpeper (2011) ameendeleza nadharia yake ya utoupole kwa kugusia dhana ya arudhi na utoupole. Anadai kwamba, msikiiizaji anaweza kubainisha kauli za kejeli na kauli ambazo siyo za kejeli kwa kusikia toni ya msemaji kwenye mazungumzo. Anaeleza kwamba, wakati mwingine siyo kauli ambayo imesemwa inaashiria utoupole bali namna ambavyo kauli hiyo imesemwa na msemaji. Katika utafiti huu, dhana ya urudhi ilitusaidia kubainisha iwapo kauli zinazotolewa na waigizaji wa filamu zilizofanyiwa utafiti huwa ni kauli zinazoashiria utoupole kwenye mazungumzo au la.

Japo wataalam hawa wanaungalia utoupole kwa kutumia mikabala tofauti, inajitokeza kuwa wote wanajifunga na mtazamo wa kiufafanuzi na kikaida katika kulikabili suala la utoupole. Aidha, mikabala yao ni tofauti lakini wanaelekea kukubaliana kuhusu kitu kimoja kuwa utoupole hutokea katika hali mbalimbali kwenye mazungumzo. Utafiti huu hata hivyo, unaongozwa na mawazo ya nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) kwa vile inahusisha kipengele cha mikakati ya utoupole ambacho ndicho msingi wa uchambuzi wa mada ya utafiti.

Kuna watafiti ambao wametumia nadharia utoupole ya Culpeper (1996) kuchunguza suala la utoupole na mikakati yake katika kuchambua matini mbalimbali. Kwa mfano, Goro (2014) alichunguza lugha ya makondakta wa daladala inavyodhihirisha utoupole kati ya abiria na makondakta. Utafiti huu ulifanywa kwenye daladala za kutoka jijini Nairobi kuelekea mtaa wa Dandora. Goro alitumia nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) kubainisha mikakati mbalimbali ya utoupole wanayotumia makondakta hao kuvunja mawasiliano kati yao na

abiria. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kwamba, mkakati chanya wa utoupole na mkakati hasi wa utoupole ndiyo mikakati ambayo inatumiwa zaidi na makondakta wa daladala hizo kudhihirisha utoupole kwenye mawasilino.

Utafiti huu pia ulibainisha sababu zinazosababisha utoupole kwenye mazungumzo kati ya abiria na makondakta na kubainisha kuwa mamlaka na mahusiano ya kijamii ndiyo sababu kuu inayochochea utoupole kwenye mazungumzo kati ya abiria na makondakta wa daladala za kutoka jijini Nairobi kuelekea mtaa wa Dandora. Utafiti uliofanywa na Goro unahusiana na utafiti huu kwa kuwa unahusisha suala la utoupole kwenye mazungumzo na pia uliendelezwa na nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996).

Tofauti kati ya utafiti uliofanywa na Goro na utafiti huu ni kuwa, utafiti huu unajikita kwenye tasnia ya filamu kwa kuchunguza suala la utoupole kwenye mazungumzo ya waigizaji kwenye filamu za Kiswahili kutoka nchini Tanzania ilhali utafiti uliofanywa na Goro ulijikita kwenye sekta ya daladala. Hata hivyo utafiti uliofanywa na Goro ulitufaa kwenye utafiti huu kwa vile unadhihirisha jinsi ambavyo nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) inavyoweza kutumiwa katika kufafanua dhana ya utoupole kwenye mazungumzo. Utafiti uliofanywa na Goro ni nguzo muhimu katika kuiwekea kazi hii msingi wa kinadharia.

Wengi wa watafiti ambao ni wa nchi za ulaya, wameitumia nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) katika kuchunguza matumizi ya lugha ya wahusika katika sinema mbalimbali. Tutazipitia baadhi ya kazi hizi kama sehemu ya madurusu. Nabelle (2015) alitumia nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) katika kuchunguza mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika wajenzi kwa mhusika mkuu katika sinema ya *Paranorman*. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa, mkakati ndani ya rekodi wa utoupole hutumiwa zaidi na wahusika wajenzi wa sinema hii kudhihirisha utoupole wanapotangamana na mhusika mkuu katika mawasiliano.

Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa, mhusika mkuu anapokabiliana na hali ya utoupole, huikabili hali hii kwa kumshambulia msemaji kwa kutenda vitendo vinavyodhuru uso wa msemaji. Pia ilibainika kuwa namna ya kukabili hali ya utoupole hutegemea jinsi ambavyo vitendo vinavyodhuru uso wa msikilizaji vimewasilishwa na msemaji au uhusiano kati ya msemaji na msikilizaji.

Utafiti uliofanywa na Nabelle unahusiana na utafiti huu ila tofauti ni kwamba, utafiti huu unajifunga kwenye filamu nne za Kiswahili za Kitanzania ilhali utafiti uliofanywa na Nabelle ilijikita kwenye sinema ya *Paranorman* ambayo ni sinema ya Ulaya. Utafiti uliofanywa na Nabelle ni muhimu katika utafiti huu kwa vile unauwekea msingi wa kinadharia. Zaidi ya hayo, utafiti uliofanywa na Nabelle unahusisha lugha ya mazungumzo baina ya waigizaji wa sinema ya *Paranorman* sawa na ilivyo kwenye mazungumzo za waigizaji wa filamu za Kiswahili zilizofanyiwa uchunguzi.

Kwa msingi huu, uainishaji wa mikakati ya utoupole uliotumika katika mazungumzo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa vile utasaidia katika kuchambua na kuanisha kauli za waigizaji katika filamu zilizoteuliwa kufanyiwa uchunguzi. Hali kadhalika, utafiti uliofanywa na Nabelle ulitusaidia kubainisha namna waigizaji wa filamu hizi wanakabiliana na hali za utoupole katika mazungumzo.

Budi (2015) alitumia nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) kuchunguza matumizi ya mikakati ya utoupole kwenye sinema za *Die Hard 3* na *The Expendables*. Matokeo ya uchunguzi yalibainisha kuwa mikakati ya utoupole inayotumiwa zaidi na waigizaji wa sinema hizi ni mkakati ndani ya rekodi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole na mkakati hasi wa utoupole. Tofauti kati ya utafiti wa Budi na utafiti huu ni kuwa, Budi alishughulikia sinema za Ulaya ilhali utafiti huu umejikita kwenye filamu nne za Kiswahili za Kitanzania.

Utafiti uliofanywa na Budi ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa unahusisha suala la utoupole kwenye mazungumzo ya waigizaji wa sinema.

Kinyua (2015) alichunguza ukiukaji wa kanuni za upole katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) kuchunguza namna ambavyo wahusika kwenye riwaya hii hukiuka kanuni za upole ili kujenga na kuendeleza maudhui kwenye riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Katika uchunguzi huu, Kinyua alipendekeza matumizi ya nadharia tofauti katika kuchunguza suala la ukiukaji wa kanuni za upole. Tofuti kati ya utafiti uliofanywa na Kinyua na utafiti huu ni kuwa utafiti uliofanywa na Kinyua uliegemea lugha andishi katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ilhali utafiti huu unaegemea lugha zungumzwa katika filamu nne za Kiswahili.

Vilevile, nadharia iliyoendeleza utafiti uliofanywa na Kinyua ni nadharia ya upole ya Brown na Levinson. Utafiti huu kwa upande mwingine uliendelezwa na nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996). Hata hivyo utafiti uliofanywa na Kinyua ulitufaa katika kueleza jinsi utoupole unabainika kwenye mazungumzo ya waigizaji wa filamu zilizoteuliwa kufanyiwa uchunguzi.

1.9.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Filamu za Kitanzania

Watafiti mbalimbali wamefanya tafiti kuhusu filamu nchini Tanzania. Mponguliana (1982) alifuatilia maendeleo ya filamu nchini Tanzania. Yeye alijikita kwenye utengenezaji wa filamu katika kipindi kabla ya ukoloni, baada ya ukoloni na baada ya uhuru. Utafiti uliofanywa na Mponguliana ulitusaidia katika utafiti huu kwa kuonyesha maendeleo ya sanaa ya filamu nchini Tanzania hususan vipindi mbalimbali ambavyo tasnia hii imepitia.

Njewe (2007) alichunguza jinsi maonyesho ya kitamaduni yanavyotumiwa kwenye filamu za Kiafrika. Anadai kwamba filamu chache sana zinaonyesha maonyesho ya utamaduni wa Mwafrika. Anapendekeza kuwa watengenezaji wa filamu wazingatie maonyesho ya kitamaduni ya Kiafrika katika filamu zao ili kuyahifadhi kwa ajili ya utambulisho na manufaa ya kizazi kijacho. Kwa kuzingatia hili, filamu inaweza kuonyesha au kutambulisha taifa fulani kwa kuangalia yale yanayoonyeshwa hasa kwa kuzingatia utamaduni wa jamii husika.

Suwed (2013) alichunguza usawiri wa kijinsia katika lugha ya filamu za Marehemu Steven Kanumba ili kubainisha namna lugha hutumiwa kusawiri masuala ya kijinsia katika jamii. Matokeo ya utafiti uliofanywa na Suwed yalibainisha kuwa marehernu Kanumba, katika filamu zake alitumia zaidi kejeli na dhihaka kuliko vipengele vingine vya lugha. Utafiti uliofanywa na Suwed unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa, utafiti huu utajikita kwenye suala la utoupole kwenye mazungumzo ya waigizaji wa filamu za Kiswahili kutoka Tanzania. Hata hivyo, kupitia kwa utafiti uliofanywa na Suwed, tutapata uelewa zaidi kuhusu tasnia ya filamu nchini Tanzania.

Shule (2014) alichunguza suala la sanaa na maendeleo nchini Tanzania. Katika uchunguzi huu, ilibainika kwamba sanaa ilitumiwa kama njia ya kuelimisha wanajamii kuhusu matatizo yanayowakumba na namna ya kukabili matatizo hayo katika kipindi cha ukoloni nchini Tanzania. Utafiti uliofanywa na Shule ulitufaa kwenye utafiti huu kwa kuelewa zaidi kuhusu sanaa hii na maendeleo yake nchini Tanzania.

Pembe (2015) alichunguza mikakati ya tafsiri na usawa wa ujumbe katika tafsiri ya mazungumzo ya Kiingereza kwenye filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Tofauti kati ya utafiti huu na utafiti uliofanywa na Pembe ni kwamba, ulijikita kwenye ukosefu wa usawa wa ujumbe katika tafsiri ya Kingereza ilhali katika utafiti huu, ulichunguza suala

la utoupole kwenye filamu za Kiswahili nchini Tanzania, kwa kujikita kwenye filamu nne tofauti ambazo zimeongozwa na wasanii tofauti. Utafiti uliofanywa na Pembe kama ulivyo utafiti uliofanywa na Suwed, utatuwezesha kuielewa tasnia ya filamu nchini Tanzania kwa kina.

1.10 Mbinu za Utafiti

1.10.1 Mbinu za Kukusanya Data

Filamu nne za Kiswahili kutoka nchini Tanzania zilitutumiwa kama data ya kimsingi. Filamu hizi zilitumiwa katika uchunguzi wa kubainisha mikakati ya utoupole inayotumika katika juhudi za kudhuru nyuso za waigizaji katika mazungumzo. Filamu ambazo ziliteuliwa kimakusudi ili kufanikisha uchunguzi huu ni: *Hila, Tabasamu Ghushi, Upepo wa Baridi na Majuto*.

Baada ya kutazama filamu hizi kwa mara kadhaa, kauli za waigizaji zinazofikiriwa kuonyesha utoupole zilinakiliwa ili kurahisisha uchunguzi wa mikakati ya utoupole inayotumiwa na waigizaji katika juhudi za kudhuru nyuso za waigizaji wengine katika mazungumzo.

1.10.2 Uteuzi wa Sampuli

Filamu zilizoteuliwa kufanikisha utafiti huu zilitolewa katika mtandao wa YouTube. Mbinu iliyotumiwa kuteua sampuli ni mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalum. Mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu ni mbinu ambayo mtafiti anaamua mwenyewe kwa hiari yake kuteua kundi la watu au vitu anavyoamini vinaweza kumpatia data inayoweza kufanikisha malengo ya utafiti wake. Mtafiti alitumia filamu kama sampuli lengwa kwa sababu filamu huhusisha lugha ya mazungumzo ambapo waigizaji kwenye filamu huzungumza kwa njia ya moja kwa moja.

Kwa msingi huu, ilikuwa rahisi kwa mtafiti kuchanganua jinsi mikakati ya utoupole inavyotumika katika juhudi za kudhuuru nyuso za waigizaji katika mazungumzo yao kwa nia ya kusababisha uhasama. Hali kadhalika, filamu husika hazijafanyiwa uhakiki mwingine unaohusiana na utoupole hadi kwa sasa.

1.10.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Baada ya kunakili kauli za waigizaji zinazofikiriwa kuonyesha utoupole, ziliaininishwa kulingana na kategoria za mkakati hasi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati ndani ya rekodi, matumizi ya kejeli, na kutowasilisha chochote. Baada ya kuzianisha kauli hizi katika kategoria za mikakati husika, kauli hizi zilifafanuliwa kwa misingi ya nadharia ya utoupole iliyoasisiwa na Culpeper (1996). Vilevile, jedwali linaloonyesha frikwensi ya matumizi ya mikakati ya utoupole katika filamu husika lilitumiwa kubaini ni mkakati upi wa utoupole unatumiwa zaidi na waigizaji wa filamu husika. Pia jedwali linaloonyesha frikwensi ya matumizi ya mbinu za kukabiliana na utoupole na wahusika wa filamu husika lilitumiwa ili kubaini ni mbinu gani inatumiwa zaidi ili kukabili suala la utoupole katika mazungumzo ya waigizaji wa filamu husika.

1.11 Muhtasari wa Sura

Sura ya kwanza ya tasnifu hii imeweka msingi wa utafiti kwa kueleza usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, upeo na mipaka ya utafiti, msingi wa nadharia ya utafiti, mbinu za kukusanya data na uwasilishaji wa data.

Sura ya pili inajadili dhana ya utopole kwa kujikita katika mitazamo ya wataalamu mbalimbali. vilevile dhana ya utopole katika mawasiliano imejadiliwa kwa kuangazia namna arudhi hasa kiimbo hudhihirisha utopole katika mazungumzo. Vilevile, hali zinazoathiri matumizi ya mikakati ya utopole katika mawasiliano zimejadiliwa.

Sura ya tatu ya tasnifu hii inafafanua matumizi ya mikakati ya utopole katika filamu husika kama ilivyopendekezwa na Culpeper (1996). Mifano mwafaka kutoka kwa filamu husika imetolewa kama inavyojitokeza kwa kauli za waigizaji wa filamu husika.

Sura ya nne ya tasnifu hii inajadili namna waigizaji wa filamu husika wanakabiliana na hali ya utopole katika mazungumzo. Sura ya tano ya tasnifu hii inajadili matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti pamoja na kutoa mapendekezo ya tafiti zijazo.

SURA YA PILI

UPOLE NA UTOUPOLE KATIKA MAWASILIANO

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, dhana ya upole itajadiliwa kwa kuangazia maoni ya watalaamu mbalimbali kama vile Lakoff (1973), Grice (1975), Fraser na Nolen (1981), Leech (1983) na Brown na Levinson (1987). Ijapokuwa utafiti huu unachunguza suala la utoupole katika filamu za Kiswahili, pana haja kubwa ya kuelewa dhana ya upole kwa sababu nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) ina msingi wake katika nadharia ya upole, hasa nadharia ya uso ya upole ya Brown na Levinson (1987). Aidha, dhana ya utoupole na suala la arudhi kama inavyoelezwa na Culpeper (2005) itajadiliwa hasa kwa kujikita katika kiimbo na namna utoupole huweza kudhihirika kwa aina mbalimbali za kiimbo. Hali kadhalika, hali zinazoathiri matumizi ya mikakati ya utoupole katika mawasiliano zitajadiliwa.

2.2 Upole

Baadhi ya wataalamu ambao wanahusishwa na dhana ya upole ni pamoja na Lakoff (1973), Grice (1975), Leech (1983), Fraser na Nolen (1981), Brown na Levinson (1987) miongoni mwa wengine. Katika sehemu hii, mitazamo minne mikuu ya watalaamu hawa itajadiliwa kwa kuelezea maoni yao kuhusu dhana ya upole.

Lakoff (1973) anaeleza kwamba watu huzingatia seti maalum ya kanuni zinazozuia kuvunjika kwa mawasiliano wanapowasiliana. Anapendekeza kanuni mbili ambazo sharti zitumiwe katika mawasiliano ili kuzuia kuvunjika kwa mawasiliano. Kanuni hizi ni kanuni ya uwazi na kanuni ya upole. Kanuni ya uwazi humtaka msemaji kusema habari za kweli kwa mujibu wa maarifa na ushahidi wake, kutozidisha habari husika, na kusema habari iliyo na mchango katika kile anachozungumzia na aseme kwa namna iliyo wazi na isiyo na utata.

Kanuni ya upole humtaka msemaji kutolazimisha msikilizaji kupokea habari yake. Humtaka msikilizaji kupokea habari ya msemaji kwa hiari yake. Kanuni hii pia humtaka msemaji kumpa msikilizaji nafasi ya kutoa maoni yake au kujibu kulingana na maoni yake. Vilevile, kanuni hii humtaka msemaji kumfanya msikilizaji ahisi kuwa anathaminiwa au ni sehemu ya mazungumzo. Ni dhahiri kuwa, kanuni ya upole ina vijikanuni vitatu vidogo ambavyo sharti msemaji azingatie ambavyo ni: asilazimishe, apatiane nafasi ya kuchagua na amfanye msikilizaji ahisi vizuri.

Lakoff (1973) anasema kwamba, katika mawasiliano, sharti msemaji ajaribu kuwianisha kanuni hizi kwa vile haziwezi zikatumiwa kikamilifu kwa wakati mmoja zikiwa zote. Hivyo basi, ni jukumu la msemaji kujaribu kuzioanisha ili zitumike kwa namna iliyo sawa hivi kwamba kila moja ya kanuni hizi inapewa nafasi yake. Anaeleza kwamba, kanuni hizi zinapokosa kutumiwa kwa namna iliyo sawa, inachukuliwa kuwa msemaji amekosa kudhihirisha upole katika mawasiliano. Kwa maoni ya Lakoff, upole hujidhihirisha katika mawasiliano mzungumzaji anapozingatia matumizi ya kanuni ya uwazi na kanuni ya upole na vipengele vyake vyote na wakati uo huo kuzisawazisha kikamilifu kwa kupatia kila moja nafasi.

2.3 Utaratibu wa Ushirikiano (Grice 1975)

Grice (1975) anaeleza kwamba ili kufanikisha mawasiliano, lazima watu waelewane. Kuelewana huku katika mawasiliano ni utaratibu wa ushirikainao. Utaratibu wa ushirikiano hutawaliwa na kanuni nne kuu ambazo ni: Kanuni ya ukweli, kanuni ya namna, kanuni ya idadi na kanuni ya uhusiano. Kanuni ya ukweli humtaka msemaji kusema mambo ambayo ana ushahidi nayo. Hivyo basi, msemaji hapaswi kusema kile ambacho anaamini ni uwongo.

Kwa upande mwingine, kanuni ya namna humtaka msemaji kusema mambo kwa njia ya wazi, kujiepusha na utata na kutosema mambo mengi kupita kiasi. Kanuni ya idadi nayo huwataka watu kusema mambo kwa idadi ifaayo. Hawapaswi kuzidisha au kupunguza. Kanuni ya uhusiano huwataka watumizi kusema habari zinazohusiana na mada au jambo linalozungumziwa.

Hata hivyo, kanuni hizi za ushirikiano wakati mwingine huwa hazizingatiwi kama sheria kwa sababu wakati mwingine msemaji hutaka kupeana habari zaidi kuhusu mada inayozungumziwa na hivyo basi kanuni ya idadi inakiukwa. Kanuni ya namna kwa upande mwingine hukiukwa wakati ambapo msemaji ananua kupitisha ujumbe kwa msikilizaji mmoja kati ya wasikilizaji wengi na hataki wasikilizaji hawa waelewe ujumbe husika. Hivyo basi, itambidi akiuke kanuni ya namna kwa kutosema mambo kwa njia ya wazi.

2.4 Upole kama Mkataba wa Mazungumzo (Fraser na Nolen 1981)

Fraser na Nolen (1981) wanaeleza dhana ya upole kama mkataba wa mazungumzo. Mkataba wa kijamii hueleza seti ya haki na majukumu ambayo msemaji na msikilizaji hupaswa kuwasilisha wakati wa mazungumzo. Watu wanapokuwa katika mazungumzo fulani, kila mshiriki huleta seti ya haki na majukumu ambayo huamua ni nini washiriki wa mazungumzo husika wanatarajia kutoka kwa kila mmoja wao. Hivyo basi, kulingana na Fraser na Nolen, upole hudhihirika katika mazungumzo wakati ambapo washiriki huzingatia kanuni za uhusiano, na hili husisitiza desturi ambazo zinakubalika na jamii. Kwa mfano, katika jamii nyingi za kiafrika, watoto hupaswa kuamkia watu walio na umri mpevu kuwaliko. Hivyo basi, upole si kitendo cha kumfanya msikilizaji ahisi vizuri, bali ni kutekeleza sheria na masharti ya mkataba wa mazungumzo.

Kutokana na maelezo ya Fraser na Nolen (1981) utoupole hudhihirika katika mazungumzo wakati ambapo sheria na masharti ya mkataba wa mazungumzo zinakiukwa. Kwa mfano, mwajiriwa anapoamrisha mwajiri wake, anakiuka kanuni za uhusiano. Hata hivyo, Fraser na Nolen wanasisistiza kwamba upole na utoupole katika mazungumzo hutegemea na maoni ya msikilizaji. Wanadai kwamba, wakati mwingine japo msemaji hulenga kudhihirisha upole katika mazungumzo, msikilizaji anaweza kufasiri hali hii kama utoupole. Hata hivyo, kinachofasiriwa kama upole au utoupole hutegemea sheria mahususi za mkataba wa mazungumzo kati ya msemaji na msikilizaji katika mazungumzo husika.

2.5 Kanuni za Upole za Leech (1983)

Leech (1983) anaangazia dhana ya upole kwa kuegemea mkabala wa kipragimatiki. Anafasiri dhana ya upole kama aina ya tabia ambayo huwawezesha washiriki katika mazungumzo kuhusika katika mtagusano wa kijamii katika hali ya kiupatano. Anadai kwamba, jambo muhimu katika mawasiliano ni kudumisha mazingira ambayo yatadumisha mawasiliano. Anazidi kueleza kwamba, mawasiliano hutawaliwa na kanuni sita kuu ambazo lazima zizingatiwe. Kanuni hizi ni: Kanuni ya mkakati, kanuni ya sifa, kanuni ya takrima, kanuni ya huruma, kanuni ya kujitweza na kanuni ya ukubaliano.

Kanuni ya mkakati hulenga kupunguza gharama kwa wengine na kujigharimu zaidi. Vilevile huhusisha kutoa miadi na kuepusha ulazimishaji. Kwa mfano, badala ya msemaji kumtuma msikilizaji moja kwa moja kwa kuamrisha kwa kusema kauli kama nenda sokoni ukanunue mboga, namna bora ya kudhihirisha upole ni kuuliza swali kama je, ninaweza kukutuma sokoni ukanunue mboga? Kanuni ya sifa kwa upande mwingine ni kanuni ambayo humtaka msemaji kumsifu msikilizaji na kumfanya ahisi kuwa anathaminiwa. Hivyo basi kauli za msemaji kwa msikilizaji sharti zisheheni sifa nyingi kwa msikilizaji. Kanuni hii vilevile

humtaka msemaji kutumia kauli zilizo na athari chanya kwa msemaji katika hali ambapo msemaji hawezi toa kauli za kumsifu msikilizaji wake.

Kanuni ya takrima humtaka msemaji kuzingatia matumizi ya maneno ya ukarimu. Hivyo basi msemaji huhitajika kupunguza maneno yenye kudhihirisha ubinafsishaji na kutumia maneno ya kutojipendelea. Hivyo basi sharti msemaji atumie kauli kama vile karibu tena nyumbani kwetu, karibu tule chakula cha mchana n.k. Kanuni ya kujitweza nayo humtaka msemaji kujidunisha na kumtukuza msikilizaji. Kwa kutoa kauli kama vile mimi si gwiji kama wewe, wewe ndiye mtalaamu. Hivyo basi kanuni hii humtaka msemaji kutojisifu bali kauli zake kwa msikilizaji sharti zidhihirishe kwamba anajitweza.

Kanuni ya huruma humtaka msemaji kumwonyesha huruma msikilizaji na kuepuka kuonyesha huruma kwake hasa katika hali ambapo msikilizaji amekubwa na majanga fulani. Msemaji anaweza kutoa kauli kama vile; pole kwa mabaya yaliyokusibu mwenzangu. Kanuni ya ukubaliano nayo humtaka msemaji kuonyesha uhusiano katika utaratibu wa kumsemesha msikilizaji kwa kujiepusha na hali ya kutosikizana na kujaribu kupalilia usikizano kwa kiwango cha juu iwezekanavyo. Hivyo basi kanuni hii humtaka msemaji kuhakikisha kwamba mawasiliano kati yake na msikilizaji hayavunjiki. Kanuni hii hudumisha uhusiano mwema kati ya msemaji na msikilizaji.

Hata hivyo, Brown na Levinson (1987) wanaeleza kwamba kanuni za upole zilizopendekezwa na Leech hasa kanuni ya kiasi haina ufafanuzi mwafaka kwa kuwa hakuelezea hasa ni kiasi gani. Pia wanadai kwamba, Leech hakuelezea iwapo kanuni hizi ni bia au zinazingatiwa na watu wa utamaduni mahsusi. Hata hivyo, watu wanapowasiliana, hujaribu kufuata kanuni hizi ili kufanikisha mawasiliano ijapokuwa katika hali ambapo msemaji ana nia ya kuzua ugomvi katika mawasiliano, basi kanuni hizi hukiukwa.

2.6 Upole kama Mkakati wa Kuokoa Uso

Brown na Levinson (1987) wanaeleza dhana ya upole kama mkakati wa kuokoa uso. Wanadai kwamba, uso lazima uzingatiwe katika mazungumzo kwa kuwa ni kitu dhaifu na katika mawasiliano uso unaweza kuumbuliwa au ukahifadhiwa. Kwa msingi huu, msemaji lazima ajaribu kudumisha sio tu uso wake bali pia uso wa msikilizaji wakati ambapo anakabiliwa na hali zinazotishia kuhasiri uso kama vile kutoa amri, kukosoa, kutokubaliwa miongoni mwa hali nyigine. Brown na Levinson wanapendekeza mikakati ya upole ambayo tumeijadili katika sura ya kwanza. Mikakati ya upole hulenga kuhakikisha kwamba uso wa msemaji na msikilizaji unahifadhiwa wakati ambapo vitendo vinavyotishia uso vinatekelezwa.

2.7 Utoupole katika Mawasiliano

Madhumuni ya lugha huwa ni kuwasiliana. Mawasiliano yanahusu kupitisha ujumbe kutoka kwenye ubongo wa msemaji hadi kwenye masikio ya msikilizaji hasa kupitia kwa lugha ya mazungumzo. Ili kufanikisha mawasiliano, lazima kuwepo na chanzo. Chanzo ni mtu anayepitisha ujumbe. Sharti ujumbe huu uwasilishwe kwa mfumo wa ishara, maandishi au mikono. Ujumbe ni zile fikra zinazowasilishwa na chanzo kwa kutumia mfumo wa ishara. Ujumbe huu hupitishwa kutoka kwa chanzo hadi kwa msikilizaji kwa njia ya sauti au kuona. Baada ya mpokeaji kupokea ujumbe kutoka kwa chanzo, basi ujumbe huu hufasiriwa na mpokeaji ili uweze kueleweka. Baada ya kufasiri ujumbe husika mpokeaji hutoa majibu kwa chanzo. Ni dhahiri kwamba mawasiliano ni mchakato ambao hauna mwanzo au mwisho.

Ili kufanikisha mawasiliano, Brown na Levinson (1987) wanaeleza kwamba mikakati ya upole hutumiwa kwa madhumuni ya kuhifadhi uso wa msemaji na msikilizaji katika hali ambazo vitendo usemi hutishia uso. Hata hivyo, Culpeper (1996) anatofautiana na mawazo ya Brown na Levinson anaposema kwamba, wakati mwingine msemaji huwa hana nia ya

kuhifadhi uso wa msikilizaji bali hunuia kuhasiri uso wa msikilizaji kwa kutenda kimakusudi vitendo vinavyohasiri uso, hali ambayo huweza kuzua ugomvi mkali kati ya msemaji na msikilizaji. Mills (2003) anakubaliana na mawazo ya Culpeper kwa kusema kwamba, katika mawasiliano, wakati mwingine huwa hakuna utaratibu wa ushirikiano na hivyo basi, msemaji huhasiri uso wa msikilizaji.

Leech (1983) anaeleza kwamba, katika mawasiliano, wakati mwingine msemaji anaweza kutoa kauli hasi kwa msikilizaji bila kauli hizo kuonyesha dhahiri kwamba ni kauli hasi. Culpeper (1996) anakubaliana na mawazo ya Leech kwa kusema kwamba, katika mazungumzo kuna vitendo usemi ambavyo huhasiri uso wa msikilizaji. Kwa mfano: kutusi, kukashifu, kutumia lugha ya vitisho n.k. Vilevile, kuna vitendo ambayo msemaji hutenda kwa lengo la kufanya mzaha wala si kwa lengo la kuhasiri uso wa msikilizaji. Hali hii inajulikana kama banta.

Culpeper (1996) alipendekeza mikakati mitano ya utoupole katika mawasiliano ambayo imejadiliwa katika sura ya kwanza. Culpeper n.w (2003) wanaeleza kwamba, msemaji anaweza kutumia mikakati miwili au zaidi ya utoupole kwa wakati mmoja au mkakati mmoja ukarudiwa. Urudiaji huu unajulikana kama usambamba na hutumiwa kwa lengo la kuonyesha msisitizo wa utoupole katika mawasilino. Hali hii hii inadhihirika wazi katika mfano huu ambao umetolewa katika filamu ya *Hila*.

2. Angel: Wewe! Liangalie linavyokula. Unajua tu kula humu ndani, hicho tu ndicho unachokiweza. Kula na umbeya...wewe si umeshindwa kuishi kwenu? Huko maisha magumu na sura lako lilivyo libaya wala hakuna mwanamume wa kukuo...pumbavu!

Kijakazi : (Kimya)

Mkakati wa utoupole uliotumiwa ni mkakati ndani ya rekodi kwa kuwa kauli ya msemaji ni dhahiri na yenye habari nzito kwa msikilizaji. Hata hivyo, mkakati chanya wa utoupole umetumika pale ambapo msemaji anamtusi msikilizajina kwamba yeye ni mpumbavu. Vilevile, mkakati hasi wa utoupole umetumika pale ambapo msemaji anamrejelea msikilizaji kwa namna hasi kwa kumwambia kwamba sura yake si nzuri na hivyo basi hafai. Tofauti na Culpeper, Brown na Levinson (1987) wanasema kwamba mikakati tofauti ya upole haipaswi kutumiwa kwa wakati mmoja.

2.8 Dhana ya Utoupole na Arudhi

TUKI (1990) wanaeleza kwamba arudhi ni neno linalojumuisha mabadiliko katika tempo, kidatu, mkazo n.k wakati wa utamkaji wa sauti za msingi. Culpeper (2005) anadai kwamba, viziada lugha au sifa za usemaji ambazo si sehemu ya mfumo wa lugha husaidia kubaini iwapo kauli zinazotolewa na wahusika katika mazungumzo zinaashiria upole au utoupole katika mazungumzo. Culpeper anazidi kueleza kwamba sifa za kiarudhi zina jukumu la kujenga na kutathimini suala la utoupole.

Culpeper (2011) anaeleza mawazo haya kwa kina kwa kusema kwamba, wakati mwingine katika mazungumzo, si kauli ambayo imesemwa inaashiria utoupole ila ni namna ambavyo kauli husika imesemwa. Anataja sifa za kiarudhi kama vile: Kiimbo, kidatu, toni, tempo n.k. Katika matumizi ya kejeli kama mkakati wa utoupole katika mawasiliano, Culpeper anadai kwamba msikilizaji anaweza kubaini kauli za kejeli na zisizo za kejeli kwa kusikiliza toni ya sauti ya msemaji.

Massamba (2004) anaeleza kwamba toni ni sifa inayowakilisha kiwango pambanuzi cha kidatu cha silabi katika neno au sentensi na ambayo huweza kubadilisha maana ya neno au sentensi hiyo kisemantiki au kisarufi. Hivyo basi, kwa msingi huu toni ni kubadilika kwa kidatu ambako hutokea katika kutamka silabi au maneno ambayo huathiri maana za maneno. TONI huweza kuwa ya juu, ya kati, ya chini, ya kupanda au kushuka.

Lugha zenye toni ni lugha ambazo hutumia kidatu na toni kubainisha maana za faridi za kileksika na uamilifu wa kisarufi. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili si lugha yenye toni, dhana ya toni na namna inavyoathiri utoupole katika mazungumzo haitajadiliwa ila utafiti huu utaangazia namna kiimbo kinavyoweza kudhihirisha utoupole katika mazungumzo.

2.8.1 Dhana ya Kiimbo na Utoupole

Kwa mujibu wa Massamba (2004) kila lugha ya binadamu huwa na utaratibu wake maalum wa upandaji na ushukaji wa mawimbi ya sauti zake. Utaratibu huu unajulikana kama kiimbo. Kiimbo ni moja ya sifa za kiarudhi na hudhihirika pale viwango vya kidatu hutumiwa katika kiwango cha sentensi katika kutofautisha maana inayosemwa. Hivyo basi, kidatu ni kipengele ambacho huandamana na kiimbo. Kidatu huelezwa kama utamkaji wa sauti ambao unaweza kuwa katika kiwango cha kati, kiwango cha chini au kiwango cha juu.

Katika mchakato wa mawasiliano, kiimbo humwezesha msikilizaji kuelewa ikiwa msemaji anatoa maelezo, anashangaa, anaamrisha, anauliza swali au anakejeli n.k. vilevile, kiimbo hutumiwa kuonyesha msimamo au nia ya mzungumzaji. Iwapo msemaji ananua kuhasiri uso wa msikilizaji kwa kutoa kauli za kejeli, kuamrisha, kutumia lugha ya vitisho n.k basi itadhihirika wazi kwenye kiimbo.

Kwa mfano:

3. Kejeli: Ati unamiliki majumba ya ghorofa ilhali walala kibandani!

Swali: Unamiliki majumba ya ghorofa ilhali walala kibandani?

Katika mfano huu, ni dhahiri kwamba kauli za msemaji zinalenga kumkera msikilizaji kwa kuwa kauli hizi zimesheheni kejeli na dhihaka. Kama anavyoeleza Culpeper (1996) msemaji anapotumia maneno ya kebehi na kejeli katika mazungumzo, hali hii hudhihirisha utoupole katika mawasilino. Hivyo basi, kiimbo humwezesha msikilizaji kubaini iwapo kauli husika zinaashiria upole au utoupole katika mawasiliano.

Vilevile, kiimbo humwezesha msikilizaji kutambua iwapo kauli ya msemaji ni amri au kauli husika zinadhihirisha matumizi ya lugha ya vitisho. Kimsingi, kuamrisha na matumizi ya lugha ya vitisho katika mazungumzo ni vitendo usemi vinavyohasiri uso. Hivyo basi, kiimbo ndicho humwezesha msikilizaji kubaini iwapo kauli husika zinadhihirisha upole au utoupole katika mazungumzo. Kwa mfano, msemaji anapotoa amri kama vile, toka hapa! Anahasiri uso chanya wa msikilizaji hasa matamano ya uso chanya wa binadamu ya kutaka kushirikishwa. Kwa upande mwingine msemaji anapotoa kauli kwa kutumia lugha ya vitisho kama vile, leo utajua cha mtema kuni, utanitambua mimi ni nani n.k, hali hii hudhihirisha utoupole utoupole katika mawasiliano. Ni dhahiri kwamba, kiimbo hutumiwa kuonyesha nia ya msemaji katika mawasiliano.

2.9 Hali Zinazoathiri Matumizi ya Mikakati ya Utoupole katika Mawasiliano

2.9.1 Tofauti za Kimamlaka kati ya Msemaji na Msikilizaji

Kwa mujibu wa Culpeper (1996) utoupole katika mawasiliano hutokea zaidi msemaji anapokuwa na mamlaka zaidi ya msikilizaji. Locher na Bousifield (2008) wanakubaliana na mawazo ya Culpeper wanaposema kwamba mamlaka ni dhana muhimu katika kujadili suala la utoupole katika mazungumzo. Dhana ya mamlaka inahusu hadhi ya mzungumzaji na msikilizaji katika mazungumzo, tabaka au nguvu za kimwili n.k. Wanaeleza kwamba, mzungumzaji anapokuwa na mamlaka zaidi ya msikilizaji katika mazungumzo, mzungumzaji humdhibiti msikilizaji wake. Zaidi ya hilo, wanadai kwamba utoupole katika mazungumzo ni njia mojawapo ya kutumia madaraka aliyonayo msemaji. Hali hii inadhihirika katika filamu ya *Tabasmu Ghushi*.

4. Baba Betha: Kaa ufikirie tena mwanangu, kama utaenda kuishi na mimi nitaacha kabisa kuleta hela za matumizi kwa sababu siwezi kuendelea kuhudumia mijitu ambayo haina faida kwangu.

Katika mfano huu, baba yake Betha anatumia mamlaka ya kiuchumi aliyonayo kuonyesha utoupole katika mazungumzo kwa kuwarejelea Batuli na Grace kwa namna hasi kwa kuwaita mijitu ambayo haina faida kwake. Baba yake Betha anatumia mkakati chanya wa utoupole katika mazungumzo haya hasa mbinu ya kutumia lugha ya matusi katika mazungumzo kwa kuwaita Grace na Batuli kuwa ni mijitu ambayo haina faida kwake. Hali hii inatokea wakati ambapo baba yake Betha, anaamua kuchua binti yake Betha ili akamlee mwenyewe bila kujali kwamba Grace na Batuli wanahitaji msaada wa kifedha kutoka kwake.

Mfano mwingine unadhihirika katika mazungumzo kati ya Bosco na Benjamin katika filamu ya *Tabasamu Ghushi*.

5. Benjamin: Kaka, naomba unisikilize.

Bosco : Sihitaji kusikiliza chochote kutoka kwako. Unafikiri una nini cha kuniambia mimi? Na iwapo utasitasita katika hali hii, sitaona ajabu kuvunja ahadi yangu niliyokupa mwanzo.

Katika mfano, Bosco anatumia mamlaka ya nguvu za kimwili na a kiuchumi kuonyesha utoupole katika mazungumzo kati yake na Benjamin. Hali hii inatokea wakati ambapo Bosco anagundua kwamba Benjamin ana uhusiano wa kimapenzi na mchumba wake. Hivyo basi anachukua hatua ya kumwonya Benjamin kuhusu uhusiano huo. Licha ya kwamba Benjamin anatumia lugha ya upole anapongea na Bosco, Bosco kwa upande wake anatumia lugha ya vitisho kwa kumwambia Benjamin kwamba, iwapo asingeacha kuwa na uhusiano na mchumba wake, basi angemtendea jambo bay asana. Vilevile, Bosco anaonyesha kwamba anamdharau Benjamin kwa kuwa ana kimo cha mwili mdogo na wala hana mali yoyote anapomwambia kwamba hana chochote cha kumwambia.

Katika filamu ya *Upepo wa Baridi*, mazungumzo kati ya Daniel na mke wake yanadhihirisha utoupole hasa hali hii ikichochoa na mamlaka ya nguvu za mamlaka alizonazo msemaji hasa nguvu za kimwili, kama inavyojitokeza katika mfano huu:

6. Daniel : Doris

Doris : Wewe! Ukome! Kwanzia leo nisisikie ukitamka hilo jina.

Katika mazungumzo haya, Doris anatumia mkakati ndani ya rekodi wa utoupole hasa kwa kutoa kauli dhahiri zisizokuwa na utata wowote kwa Daniel. Matumizi ya mkakati huu wa utoupole na Doris yanachochewa na hali ya mamlaka ya nguvu za kimwili aliyonayo Doris kwa kuwa ana uwezo wa kutembea ilhali mume wake ni mlemavu.

2.9.2 Utoupole na Mahusiano ya Kijamii

Culpeper (1996) anasema kwamba utoupole hutokea kwa kiwango kikubwa kati ya watu ambao huwa na uhusiano wa karibu kuliko watu ambao wana uhusiano wa mbali. Kwa mfano, utoupole unaweza kutokea zaidi kati ya mume na mke kwa kuwa uhusiano wao ni wa karibu sana. Hali kadhalika, mume na mke hufahamiana vizuri na namna ambavyo mmoja wao anaweza kuudhi mwingine. Vilevile, wanafahamu namna ya kutulizana mmoja wao anapokuwa ameuadhika. Mfano huu umetolewa katika filamu ya *Hila*.

7. Mzee Majuto: ...ninachotaka mimi leo, wewe na watoto wako sitaki kuwaona hapa nyumbani. Nimechoka! Nimechoka! Nimechoka! Nimekuwa mnyenyekevu na mvumilivu kwako kumbe unanifanyia vituko vya ajabu. Unanisaliti!

Dotinata: Nichunguze kwanza mume wangu.

Mzee Majuto: Hapana! Sikuhitaji...

Katika mfano huu, kauli za Mzee Majuto kwa mke wake zinadhihirisha utoupole hasa Mzee Mjuto anapotumia mkakati chanya wa utoupole hasa mbinu ya kutotaka kujihusisha na msikilizaji. Mzee Majuto anaposema kwamba hahitaji mke wake, ni dhahiri kwamba hataki kujihusisha naye. Kauli hii inahasiri uso chanya wa Dotinata hasa matamano ya uso chanya wa binadamu ya kutaka kukubalika jinsi alivyo kama sehemu ya kundi la jamii.

Mfano mwingine unadhihirika katika mazungumzo kati ya Rita na Irine katika filamu ya *Majuto* kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

8. Irine: Wewe kijibwa wewe! Acha kuniropokea.

Rita : Umeanza lini kunijibu kwa namna hiyo?

Katika mazungumzo haya kati ya dada hawa wawili, ni dhahiri kwamba kauli zao zinadhihirisha utoupole katika mazungumzo. Irine anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa mbinu ya matumizi ya lugha ya matusi anapomrejelea Rita kama kijibwa. Isitoshe, Rita anakabiliana na hali hii kwa kutaka kuzua ugomvi zaidi kati yake na Irine. Hali hii inatokea wakati ambapo Rita anagundua kwamba Irine ameanza tabia ya kutoka nyumbani na kutorejea kwa wakati unaofaa.

2.10 Hitimisho

Katika sura, ni bayana kwamba uvurugaji wa upole katika mawasiliano ni suala ambalo ni vigumu kuliepuka. Imebainika kwamba, hali mbalimbali ya kijamii husababisha watu kutumia mikakati tofautitofauti ya uvurugaji wa upole. Hali hizo ni pamoja na mamlaka, uhusiano kati ya msemaji na msikilizaji, tabaka miongoni mwa hali zingine. Vilevile, ni dhahiri kwamba dhana ya arudhi hasa kiimbo ni muhimu sana katika kutofautisha kauli zinazodhihirisha upole na zile ambazo zinavuruga upole katika mawasilino.

SURA YA TATU

MATUMIZI YA MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA FILAMU ZA KISWAHILI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii, matumizi ya mikakati ya utoupole katika filamu husika itajadiliwa. Filamu hizi ni : *Hila*, *Tabasamu Ghushi*, *Upepo wa Baridi* na *Majuto* ambazo sinopsia zake zimeelezwa. Filamu hizi ziliteuliwa kimakusudi ili zitupe data iliyoweza kufanikisha malengo ya utafiti huu. Kauli za waigizaji wa filamu husika zinazoashiria utoupole katika mazungumzo zitachanganuliwa kwa msingi wa nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996). Mikakati ya utoupole inayotumiwa na waigizaji wa filamu hizi pamoja na kategoria zake mbalimbali zinazotumiwa kuhasiri uso itajadiliwa kwa kina na kutolewa mifano mwafaka kutoka kwa filamu husika. Jedwali linaloonyesha frekwensi ya matumizi ya mikakati ya utoupole katika kila filamu litatumiwa ili kubaini ni mkakati upi wa utoupole unatumiwa zaidi na waigizaji wa filamu husika.

3.2 Sinopsia ya Filamu ya *Upepo wa Baridi*

Filamu ya *Upepo wa Baridi* ni filamu ya kuisimua ambayo anaangazia ukosefu wa uvumilivu kati ya wanandoa na namna ambavyo unaweza kusababisha madhara makubwa katika asasi ya ndoa. Filamu hii inahusisha mhusika Doris ambaye anaolewa na Daniel punde tu anapohitimu masomo yake ya chuo kikuu licha ya dada yake Doris ambaye anaitwa Batuli kupinga ndoa yao kwa msingi kwamba Daniel hana ajira ambayo kipato chake kitaweza kukimu mahitaji ya familia yake. Hata hivyo, Daniel anabahatika kupata ajira ambayo kipato chake kinaweza kukimu mahitaji yao. Kwa bahati mbaya, asuhuhi moja Daniel anapoelekea kazini anapatwa na ajali mbaya ya barabarani inayosababisha miguu yake yote kulemaa.

Doris anachukua likizo kutoka kazini ili ahudumie mume wake aliyelemaa. Alex ambaye ni mwajiri wa Doris anaajiri Rachel kazi ili achukue nafasi ya Doris. Isitoshe, Rachel na Alex wana uhusiano wa kimapenzi. Mwanzoni, Doris anahudumia mume wake vizuri na hela za matumizi ya nyumbani zinapokosa anaomba msaada kutoka kwa Batuli. Bautuli anakataa kumpa msaada ila anampa ushauri wa kurudia kazi yake ya awali. Doris anaporudia kazi yake ya awali, anaanza uhusiano wa kimapenzi na mwajiri wake. Hata hivyo, tabia yake inabadilika kiasi kwamba anamtelekeza mume wake.

Rachel anapogundua kwamba Alex ana uhusiano wa kimapenzi na Doris, anaamua kulipiza kisasi kwa Alex kwa kuwa anahisi kwamba Alex amemsaliti. Rachel anachukua hatua ya kumtoa uhai Alex anapowafumana ofisini kwake wakiwa na Doris. Doris anapojaribu kutoroka ghadabu ya Rachel, anagongwa na gari na ajali hii inasababisha Doris kulemaa miguu yake. Awali, Daniel alifanyiwa upasuaji na kutembea tena. Daniel anapomtembelea Doris hospitalini, anamsamehe kwa mabaya yote aliyomtendea. Doris anapotoka hospitalini, anajitoa uhai kwa sababu anashidwa kustahimili aibu kutokana na namna ambavyo alimtesa mume wake.

3.3 Sinopsia ya Filamu ya *Hila*

Filamu ya *Hila* ni filamu ambayo inaangazia namna ambavyo wivu kutoka kwa ndugu na jamaa unavyoweza kusababisha ndoa kutibuka. Filamu hii inahusisha mhusika Dotinata ambaye ameolewa na mwanamume tajiri. Dotinata na mume wake ambaye anajulikana kama Mzee Majuto, wanafanikiwa kupata watoto wawili; mmoja wa kike na mwingine wa kiume. Tarzan, ambaye ni mtoto wa kiume wa Mzee Majuto ana rangi ya ngozi na nywele inayofanana na ya mwarabu.

Kwa kuwa dada yake Dotinata anamwonea wivu Dotinata kwa kumiliki majumba nay a kifahari, anaamua kumwambia Mzee Majuto habari za uongo kwamba Dotinata ana uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengine na hata Tarzan si mtoto wake. Mzee majuto anachukua hatua ya kuwafukuza mke wake na watoto wake. Dotinata anahangaika sana kuwalea watoto wake lakini kwa sababu ya juhudi zake, anafanikiwa tena kupata mali hali ambayo inapelekea dada yake kumwonea wivu zaidi na kuamua kuwapa watoto wa Dotinata dawa za kulevya. Tabia ya watoto wake Dotinata inabadilika sana kiasi kwamba wanamgeuka mama yao. Dada yake Dotinata anampa ushauri kwamba, wakienda kwa mganga, basi shida zake zote zitatatuliwa. Kwa kuwa dada yake ni mlaghai, anapanga njama na waganga ya kumtapeli Dotinata kiasi kikubwa cha hela.

3.4 Sinopsia ya Filamu ya *Majuto*

Fialmu ya *Majuto* ni filamu inayoangazia namna ambavyo chuki kati ya dada wawili wa toka nitoke inapelekea mmoja wao kumtoa uhai dada yake. Filamu hii inawahusisha wahusika Rita na Irine ambao wanalelewa na mama yao pekee baada ya baba yao kuaga dunia wakiwa bado wachanga. Irine ambaye ni mdogo kwa Rita anafanikiwa kupata ajira ambayo kipato chake kinasaidia kukimu mahitaji yake, mama yake na dada yake mkubwa. Rita kwa upande mwingine anakosa ajira licha ya juhudi zake za kutafuta kazi. Hivyo basi anaamua kukaa nyumbani ili asaidie mama yake kazi za ndani.

Mwanzoni, Irine anashughulikia mahitaji ya familia lakini anagundua kwamba mchumba wa Rita ambaye anaitwa Elvin ndiye mwanamume ambaye ana uhusiano wa kimapenzi naye. Irine anakerwa na usaliti huu, hali ambayo inapelekea kumchukia dada yake kiasi kwamba anakataa kuwasaidia mama yake na dada yake hela za matumizi. Rita anapotaka kumtambulisha mchumba wake kwa mama yake, Irine anaamua kumzuia Elvin kufika

nyumbani kwao kwa kumtishia kwamba angemwambia dada yake kuhusu uhusiano wao iwapo angejaribu kwenda kutambulishwa kwa mama yao. Baada ya muda mrefu, Rita anagundua kwamba Elvin ana uhusiano wa kimapenzi na Irine na tayari Irine ana ujauzito wa Elvin. Rita anachukua hatua ya kumtoa uhai dada yake.

3.5 Sinopsia ya Filamu ya *Tabasamu Ghushi*

Filamu ya *Tabasamu Ghushi* ni filamu inayoangazia mhusika Grace ambaye anapata ujauzito akiwa katika shule ya upili hali inayopelekea Grace kuachishwa shule. Wazazi wake wamafukuza nyumbani na anapoenda kumweleza Nashon ambaye ana husika na ujazito huo, Nashon anamkana. Grace anajifungua mtoto wa kike ambaye anaitwa Batuli. Katika harakati za kutafuta ajira ili aweze kukimu mahitaji ya mtoto wake, anakutana na mwanamume tajiri ambaye anaanza uhusiano wa kimapenzi naye. Grace anagundua kwamba ana ujauzito. Anajifungua mtoto wa kike anayeitwa Betha.

Betha anapokua, baba yake anamchukua ili akaishi naye huku Batuli wakibaki katika mtaa wa mabanda wakihangaika na hali ya maisha magumu. Batuli anaamua kufanya kazi za ndani ili aweze kukimu mahitaji yao. Kwa bahati nzuri, anakutana na Bosco ambaye anaamua kubadilisha hali yao ya maisha. Bosco anaamua kuwahamisha Batuli na mama kwenda katika nyumba ya kifahari na kuamua kumlipia karo ya shule na wanakubaliana kwamba, atakapohitimu watafunga ndoa. Batuli anapofika katika chuo kikuu, anakutana na Benjamin ambaye anaanza uhusiano wa kimapenzi naye. Kwa bahati mbaya, Benjamin ameathiriwa na virusi vya UKIMWI. Bosco anagundua kwamba Batuli ana uhusiano wa kimapenzi na Benjamin. Anamshauri Batuli akapimwe na majibu yanaonyesha kwamba pia Batuli ameathirika na ugonjwa wa UKIMWI.

3.6 Matumizi ya Mkakati Ndani ya Rekodi wa Utoupole

Kwa mujibu wa Culpeper (1996) mkakati ndani ya rekodi wa utoupole hutumiwa zaidi na watu walio na uhusiano wa karibu. Mkakati huu unadhihirika katika hali ambapo msemaji hutoa kauli za dhahiri zisizokuwa na utata wowote. Kauli hizi hutolewa kwa lengo la kuhasiri moja kwa moja uso wa msikilizaji. Hali hii inajitokeza katika filamu ya *Hila* katika mfano ufuatao:

9. Mzee Majuto: Hili suala halina ubishi...toka uende! Toka nje!

Dotinata: Mume wangu, unataka niondoke na watoto niende wapi?

Katika mfano huu, kauli inayotolewa na Mzee Majuto ni dhahiri na ambayo haina utata wowote. Hali hii inatokea baada ya dada yake Dotinata kumweleza Mzee Majuto kwamba mke wake ana uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengine. Dotinata anaporudi nyumbani baada ya kazi, anagundua kwamba mume wake hana furaha. Anapotaka kujua ni nini kinachomsibu, mume wake anamweleza kwa sauti ya ukali kwamba anamsaliti kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengine, kisha anamwarisha Dotinata atoke nyumbani kwake. Msemaji anapotoa kauli za kuamrisha katika mazungumzo hasa kwa sauti inayodhihirisha ukali ni kitendo kinachohasiri uso wa msikilizaji.

Katika filamu ya *Tabasamu Ghushi*, kuna matumizi kadhaa ya mkakati ndani ya rekodi wa utoupole. Wasemaji hutoa kauli za moja kwa moja zinazolenga kuhasiri nyuso za wasikilizaji wao. Vilevile matumizi ya mkakati ndani ya rekodi katika filamu hii yamechochewa na tofauti za kimamlaka kati ya msemaji na msikilizaji.

Hali hii inadhihirika katika mazungumzo kati ya Grace na Mzee Kagomba kama inavyojitokeza katika mfano huu:

10. Grace: Naomba univumilie kidogo tu.

Mzee Kagomba: Nikuvumile? Sasa mimi ndiye Kagomba wa Kagomba. Natoka, nitarudi leo hii. Utakapona sura yangu, nikute vitu viko nje au kodi yangu...

Katika mfano huu, Mzee Kagomba anamwamrisha Grace alipe kodi ya nyumba. Hali hii ilitokea wakati ambapo Grace alikuwa amepatwa na maradhi na kwa sababu ya hali yake ya umaskini hangeweza kukimu mahitaji ya kimsingi kama vile kulipa kodi ya nyumba na kununua dawa kwa ajili ya matibabu. Kwa kuwa Mzee Kagomba ndiye anamiliki nyumba aliyokuwa amepanga Grace, anatumia mamlaka ya nguvu za kiuchumi aliyonayo kutoa kauli ambazo zinadhihirisha utoupole katika mazungumzo. Kama anavyodai Leech (1983) katika hali kama hii, msemaji anapaswa kuonyesha huruma kwa msikilizaji hasa ikizingatiwa kuwa hali ya afya ya Grace haikuwa nzuri. Lakini ni dhahiri kwamba Mzee Kagomba haonyeshi huruma yoyote kwa Grace.

Mfano mwingine unadhihirika katika mazungumzo kati ya Betha na Grace kama inavyojitokeza katika mfano huu:

11. Grace: ...ukishiba, ukusanye vyombo ukaoshe.

Betha: Nikaoshe? Siwezi kuosha vyombo

Katika mfano huu, ni dhahiri kwamba Grace anatoa kauli ya kuamrisha Betha aoshe vyombo. Katika hali ya kawaida, Grace anapaswa kutumia kanuni ya mkakati wa kuepusha ulazimishaji. Betha kwa upande mwingine anatoa kauli inayodhihirisha kwamba hakubaliani na kauli ya Grace na hivyo basi anatoa kauli dhahiri inayosababisha hali ya kutosikizana kati yake na Grace.

Katika filamu ya *Upepo wa Baridi*, matumizi ya mkakati ndani ya rekodi wa utoupole yanadhihirika katika hali kadhaa. Kwa mfano:

12. Doris : ... huu ni mwisho wa mwezi sasa, ndani ya nyumba hakuna pesa ya maji, hakuna pesa ya umeme. Hata pesa ya majukumu madogo imekushinda! Unategemea nini? Na wewe nakuona uko huko tu hueleweki.

Daniel : Mke wangu Doris, una nini?

Katika mfano huu, kauli ya Doris inadhihirisha utoupole katika mazungumzo kati yake na mume wake kwa kumwambia kwamba majukumu ya kutunza familia yamemshinda na hafanyi lolote ili kurekebisha hali hii. Doris anamweleza mambo haya kwa ukali bila kuzingatia ukweli kwamba Daniel alilemaa miguu baada ya kupata ajali ya barabarani na hivyo basi hawezi kukimu mahitaji ya familia yake.

Katika filamu ya *Majuto*, matumizi ya mkakati ndani ya rekodi wa utoupole yanadhihirika kwenye kauli za wahusika mbalimbali hasa matumizi ya mkakati huu yakichochea na mamlaka aliyonayo msemaji kwa msikilizaji. Kwa mfano:

13. Mama Rita : ...hata hatusalimiani?

Rita: Wewe mama, tangu nikiwa mchanga hadi nimefika hapa, bado hujachoka na hizo shikamoo?

Katika mfano huu, kauli ya Rita kwa mama yake inahasiri uso wa mama yake. Katika hali ya kawaida, mtoto hupaswa kuonyesha heshima kwa wazazi wake, lakini Rita haonyeshi heshima kwa mama yake anapomjibu kwa namna hii. Kwa kuwa Rita ana nguvu za mamlaka ya kiuchumi, anamjibu mama yake kwa namna anavyotaka bila kuzingatia kwamba mama yake anastahili heshima. Hali hii inatokea wakati ambapo mama yake Rita anaonyesha kumpendelea Irine badala ya Rita.

3.7 Matumizi ya Mkakati Chanya wa Utoupole

Culpeper (1996) anaeleza kwamba, mkakati chanya wa utoupole hutumiwa ili kuhasiri uso chanya wa msikilizaji. Mkakati huu hudhirika katika hali ambapo msemaji anatumia lugha ya matusi, matumizi ya maneno mwiko kwenye mazungumzo, msemaji kutotaka kujihusisha na msikilizaji na msemaji kumpa msikilizaji utambulisho usiofaa. Katika filamu nne ambazo zimeteuliwa kufanisha uchunguzi huu, matumizi ya mkakati chanya wa utoupole yanadhihirika katika hali ambapo msemaji anatumia lugha ya matusi, msemaji kutotaka kujihusisha na msikilizaji na msemaji kumpa msikilizaji utambulisho usiofaa.

3.7.1 Matumizi ya Lugha ya Matusi

Matumizi ya lugha ya matusi katika filamu ya *Hila* yanadhihirika katika hali kadhaa hasa yakichochea na nguvu za mamlaka kati ya msemaji na msikilizaji kama inavyojitokeza katika mfano huu:

14. Angel: ...sura lako lilivyo libaya wala hakuna mwanamume wa kukuo...utaondoka humu ndani. Pumbavu!

Kijakazi : (kimya)

Katika mfano huu, Angela anahasiri uso chanya wa Kijakaza, hasa matamania ya uso chanya wa binadamu ya kutaka kukubalika katika jamii jinsi alivyo. Anamwambia kwamba sura yake ni mbaya na hivyo basi hatapata mwanamume wa kumwoa. Isitoshe, anamtusi kwamba yeye ni mpumbavu. Angela anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa mbinu ya matumizi ya lugha ya matusi katika mazungumzo kwa kuwa ana mamlaka ya nguvu za kiuchumi kwa sababu Kijakazi ni mwajiriwa wa kazi za ndani katika nyumba yao Angel. Hali hii inatokea wakati ambapo Angel na Tarzan wanagundua kwamba Kijakazi amemjulisha mama yao kuhusu njama yao ya kutaka kuiba pesa na kuondoka nyumbani kwao.

Matumizi ya lugha ya matusi yanajitokeza katika filamu ya *Tabasamu Ghushi* huku matumizi ya mkakati huu yakichochea na mahusiano ya kijamii kati ya msemaji na msikilizaji kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

15. Nashon : Mpumbavu wewe! Hivi unafikiri nani wa kulaumiwa? Uliwezaje kushika mimba wakati unajua kwamba wewe ni mwanafunzi?

Grace : Nashon, wewe huna sababu ya kunilaumu...

Nashon anamtusi Grace kwamba yeye ni mpumbavu kwa kushika mimba ilhali yeye bado ni mwanafunzi. Kitendo cha Nashon cha kumtusi Grace kinahasiri uso chanya wa Grace hasa matamania ya uso chanya wa binadamu ya kutaka kukubalika jinsi alivyo, kwa kuwa Nashon anakataa kumkubali Grace katika hali yake ya ujauzito. Matumizi ya mkakati huu

yanachochea na uhusiano wa karibu walionao Grace na Nashon. Hali hii inatokea wakati ambapo Grace anafukuzwa shuleni kwa sababu ya ujauzito wake. Anapomtembelea Nashon ofisini mwake, anatarajia kwamba Nashon atamwonea huruma kwa kuachishwa shule badala yake Nashon anamtusi Grace.

Katika filamu ya *Upepo wa Baridi*, matumizi ya lugha ya matusi yanabainika wazi kwenye mazungumzo kati ya Daniel na mke wake Doris. Doris anapotamauka na kuona kwamba mume wake aliyelemaa amekuwa mzigo kwake na hawezi kufanya kazi yoyote, anatumia lugha ya matusi kuonyesha kwamba amechoka na hali ya ulemavu ya mume wake. Doris anahasiri uso chanya wa Daniel kwa kumtusi kwamba yeye ni mbwa. Hali hii inajitokeza katika mazunguzo haya:

16. Daniel : Unaniumiza mke wangu.

Doris : ...sijui nikutupe wapi mbwa wewe.

Hali hii inatokea wakati ambapo Doris anarejea nyumbani kutoka kazini na kuamua kupumzika chumbani. Usiku unapofika, Daniel anaomba msaada kutoka kwa mke wake kwamba amweke kitandani ili naye pia apumuzike. Badala yake Doris anamsukuma mume wake kwa hasira na kumtusi. Doris anapaswa kuonyesha huruma kwa mume wake kwa sababu ya ulemavu wake badala yake anamtusi na hivyo basi, anakataa kumkubali Daniel katika hali yake ya ulemavu.

Katika filamu ya *Majuto*, matumizi ya lugha ya matusi yanadhihirika katika mazungumzo kati ya Irine na dada yake Rita. Rita anaporudi nyumbani usiku wa manane, Irine anapomfungulia mlango wanabishana na hali hii inapelekea Irene kumfungia nje dada yake ambaye anakasirika na kuanza kutusi Irine na mama yake kama inavyodhihirika katika mfano huu:

17. Rita : Nye kunguni fungua mlango. Mbuzi nyie.

Irine : Mama, unasikia matusi ya Rita?

Katika mazungumzo haya, ni dhahiri kwamba Rita anahasiri uso chanya wa Irine na mama yake kwa kuwatusi kwamba wao ni kunguni. Rita anawatusi kwamba wao ni kunguni kwa sababu hawawezi kukimu mahitaji yao ya kila siku kwa sababu hawana ajira, badala yake wanamtegemea Rita. Sawa na kunguni anavyotegemea damu ya mwadamu ili aishi, ndivyo Irine wanavyotegemea kipato cha Rita. Isitoshe, Rita anawatusi kwamba wao ni mbuzi. Kwa kawaida, mbuzi ni mnyama msumbufu sana na hivyo ndivyo Rita anavyowaona Irine na mama yake kwamba ni wasumbufu. Hivyo basi, Rita anahasiri uso chanya wa Irine na mama yake kwa kukataa kuwakubali katika hali yao ya ukosefu wa ajira.

3.7.2 Msemaji Kutotaka Kujihusisha na Msikilizaji

Hali ambazo wasemaji wanatoa kauli ambazo zinaonyesha kwamba hawataki kujihusisha na wasikilizaji wao zinajitokeza katika filamu husika. Kwa mfano, katika filamu ya *Hila* Mzee Majuto anapopata habari kwamba mke wake anamsaliti kwa kutoka nje ya ndoa, anamwambia mke wake kwamba hamuhitaji tena kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

18. Dotinata : Si kila binadamu anapenda jinsi tunavyoishi...

Mzee Majuto : Mimi sikuhitaji kabisa.

Kauli ya Mzee Majuto kwa mke wako inadhihirisha kwamba hataki uhusiano wowote na Dotinata. Mzee Majuto anahasiri uso chanya wa Dotinata hasa matamanio ya uso chanya wa binadamu ya kutaka kutambulika kama sehemu ya kundi la jamii kwa kuvunja ndao kati yake na Dotinata. Mzee Majuto anavunja uhusiano kati yake na mke wake bila kuchunguza kwa

kina habari alizopokea kutoka kwa shemeji yake kwamba Dotinata ana uhusiano kwa kimapenzi na wanaume wengine na hata mtoto wake wa kiume aliye na ngozi ya mwarabu si wake.

Mfano mwingine unajitokeza katika mazungumzo kati ya Nashon na Grace katika filamu ya *Tabasamu Ghushi* ambapo Grace anapomwambia Nashon kwamba amefukuzwa shule kwa sababu ana ujauzito wake, Nashon anatoa kauli ambayo inaonyesha kwamba hataki kujihusisha na Grace tena. Hali hii inajitokeza katika mazungumzo haya:

19. Grace : Ingebidi wewe na mimi tukae pamoja tushauriane kitu cha kufanya.

Nashon : Sina muda mchafu wa kukaa na wewe kujadili vitu kama hivyo...

Kauli ya Nashon kwa Grace inaonyesha kwamba Nashon hataki kuendelea kuwa na uhusiano wowote na Grace baada ya kupata ujauzito. Nashon anahasiri uso chanya wa Grace kwa kukataa kumkubali jinsi alivyo badala yake anamwambia Grace kwamba hawezi kutenga muda ili wajiadiliane kuhusu jambo la kufanya kusuhu ujauzito huo.

3.7.3 Msemaji Kumpa Msikilizaji Utambulisho Usiofaa

Hali ambazo msemaji anampa msikilizaji utambulisho usiofaa katika filamu husika zinajitokeza katika mazungumzo ya wahusika mbalimbali. kwa mfano, katika filamu ya *Hila*, Dotinata anapewa utambulisho usiofaa na dada yake kama inavyojitokeza katika mfano huu:

20. Dada yake Dotinata : Mama yenu huko nje anaitwa malaya. Anagharamia

huko nje kupita maelezo. Ananuka huko nje, hafai.

Angel : Wewe mama mdogo una yako...

Katika mfano huu, dada yake Dotinata anamtambulisha Dotinata ambaye ni mama yake Angel kama mwanamke mwenye tabia ya uzinzi. Anahasiri uso chanya wa Dotinata kwa kuwaelezea watoto wa Dotinata kwamba mama yao ni mwasherati. Hali hii inatokea wakati ambapo Dotinata anafanikiwa kupata mali nyingi baada ya ndoa yake kutibuka kutokana na habari za uongo ambazo dada yake alimwambia mume wake. Dada yake anazidi kupanga njama ya kufanya watoto wake wamgeuke. Katika mazungumzo haya, dada yake Dotinata anavunja kanuni ya ukweli kwa kusema habari ambazo anaamini ni uwongo.

Mfano mwingine unajitokeza katika filamu ya *Upepo wa Baridi* katika mazungumzo kati ya Doris na dada yake Batuli, ambapo Batuli anampa Doris utambulisho usiofaa baada ya mume wake Doris kupata ajali na kulemaa miguu. Doris anapoenda kuomba msaada kwa Batuli, anapewa utambulisho usiofaa kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya;

21. Doris : ...lakini dada, kumbuka mimi ni mdogo wako na una haki ya kunisaidia.

Batuli : Sikiliza nikwambie wewe kikaragosi, hapa kwangu hakuna msaada...

Katika mfano huu, Doris anapewa utambulisho usiofaa anapoitwa kikaragosi na dada yake Batuli. Katika hali hii, Batuli anapaswa kumwonea dada yake huruma kwa masahibu yaliyomkumba badala yake anampa unamwambia kwamba yeye ni kikaragosi. Batuli anahasiri uso chanya wa Doris kwa kumpa utambulisho usiofaa hasa kwa kumtambulisha kama kibaraka cha mume wake.

Mfano mwingine unajitokeza katika filamu ya *Majuto* katika mazungumzo kati ya Rita na mama yake. Rita anawapa dada yake na mama yake utambulisho usiofaa kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

22. Mama Rita: ... mtoto niliyemzaa hawezi kuitwa kinyago...

Rita : Irine ni kinyago, na vilevile unaweza ukawa kinyago pia...

Mazungumzo haya yanatokea wakati ambapo mama yake Irine na Rita anajaribu kuleta uelewano kati ya watoto wake kwa kumbia Rita kwamba azungumze na Irine ili waweze kutatua tofauti kati yao. Rita kwa upande mwingine hataki kuongea na Irine kwa sababu anamchukia dada yake. Hivyo asi, Rita anahasiri uso chanya wa mama yake kwa kumwambia kwamba yeye ni kinyago.

3.8 Matumizi ya Mkakati Hasi wa Utoupole

Culpeper (1996) anaeleza kwamba mkakati hasi wa utoupole hutumiwa ili kuhasiri uso hasi wa msikilizaji. Matumizi ya mkakati huu hudhihirika msemaji anapomdhihaki au kukebehi msikilizaji, msemaji kumhusisha msikilizaji na uhasi na msemaji kuingilia faragha ya msikilizaji.

3.8.1 Matumizi ya Kebehi

Kukebehi ni kuambia mtu maneno ya kuudhi kwa masihara. Hali hii inajitokeza katika kauli za waigizaji wa filamu husika. Kwa mfano, katika filamu ya *Hila Mima* na Tabitha wanamkebehi Tarzan kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

23. Tarzan : Mimi naitwa Tarzan, sijui wenzangu mwaitwa nani?

Mima: ...mambo ya kujuana majina tena vipi? Unataka kutupeleka kwa mganga?

Tabitha : Nashangaa.

Mazungumzo haya yanafanyika wakati ambapo Tarzan anaenda kwenye mkahawa na kukutana na Tabitha na Mima. Tarzan anajitambulisha na kuwaomba wasichana hawa pia wajitambulishe. Mima anamkebehi Tarzan kwa kumwambia kwamba anataka kufahamu

majina yao ili awapeleke kwa mganga. Mima anahasiri uso hasi wa Tarzan hasa matamaniao ya uso hasi wa binadamu ya kutotaka kuingiliwa.

Katika filamu ya *Tabasamu Ghushi*, matumizi ya kebehi yanajitokeza katika mazungumzo kati ya Batuli na dada yake Betha kama inavyojitokeza katika mfano huu:

24. Betha : ...muda wowote wewe ni kitabu na kalamu. Huchoki?

Batuli : Huu ni mstakabali wa maisha yangu. Kwa hivyo lazima niweke mkazo.

Betha : Ukweli, lakini nafikiri hutaki kurudia ile kazi yako ya kuwa *house girl*.

Katika mfano huu, Betha anakebehi Batuli kwa kumwambia kwamba sababu kuu ambayo anatia bidii masomoni ni kuepuka kurudia kufanya kazi za ndani kama alivyokuwa hapo awali kabla ya kupata ufadhili kutoka kwa mchumba wake Bosco. Betha anahasiri uso hasi wa Batuli kwa kumwingilia hasa aina ya kazi aliyokuwa akifanya hapo awali.

3.8.2 Msemaji Kumhusisha Msikilizaji na Uhasi

Kuna hali kadhaa katika filamu husika ambapo msemaji anahusisha msikilizaji na uhasi. Kwa mfano katika filamu ya *Majuto* hali hii inajitokeza kwenye mazungumzo kati ya Elvin na Rita.

25. Elvin: Hivi unajua wewe mwanamke ni mbishi? Kichwa chako ni kigumu sana...

Rita : Unaniitaje mimi?

Katika mfano huu, Elvin anamwambia Rita kwamba ni mbishi na haelewi mambo. Hali hii inatokea Rita anapomtembelea Elvin nyumbani kwake bila kumtaarifu, ambapo hapo awali Elvin alikuwa amemweleza kwamba asiwahi kumtembelea nyumbani kwake bila kumjulisha.

Tabia ya ubishi ni tabia hasi na kawaida bidadamu huwa hataki kuhusishwa na tabia hasi. Elvin anahasiri uso hasi wa Rita kwa kumwambia kwamba anapenda sana ubishi.

Mfano mwingine unadhihirika katika filamu ya *Hila* kama inavyojitokeza katika mazungumzo kati ya Kijakazi na Angel wakati ambapo Kijakazi anamweleza mama yake Angel na Tarzan kuwa watoto wake wanatumi dawa za kulevya na wanapanga kumtoa uhai kama inavyojitokeza katika mfano huu:

26. Angel: Hivi wewe , unajua kwamba unajua sana umbeya?

Kijakazi : (Kimya)

Katika mfano huu, Angel anamhusisha Kijakazi na tabia hasi ya umbeya. Tabia ya umbeya ni tabia ya mtu kutoa habari bila ya kutumwa na binadamu huwa hataki kuhusishwa na tibia hasi kama hii. Hivyo basi, Angel anahasiri uso hasi wa Kijakazi kwa kumwita mbeya.

3.8.3. Msemaji Kuingilia Faragha ya Msikilizaji

Katika filamu zilizofanyiwa uchunguzi, kuna hali mbalimbali ambazo wasemaji wanaingilia faragha ya wasikilizaji wao. Kwa mfano katika filamu ya *Majuto*, hali ya msemaji kuingilia faragha ya msemaji inajitokeza katika mazungumzo kati ya Mzee Majuto na Dotinata katika mfano huu:

27. Mzee Majuto: ...umetoka wapi saa hizi?

Dotinata : Kwani sikuwa nimekwenda kwenye shughuli zangu mume wangu?

Mzee Majuto : Kumbe unakingine unachokifanya kwingine?

Katika mfano huu, Mzee Majuto anaingilia faragha ya mke wake kwa kutaka kujua alikotoka. Zaidi ya hayo, anamshuku mke wake kwamba anafanya shughuli zingine kisiri bila yeye kujua. Hali hii inatokea baada ya dada yake Dotinata kumwelezea Mzee Majuto kwamba mke wake anasaliti ndoa yao. Hizi ni juhudi anazofanya dada yake Dotinata ili kuhakikisha kwamba anavunja ndoa ya dada yake.

Mfano mwingine unadhihirika katika filamu ya *Tabasamu Ghushi* katika mazungumzo kati ya Benjamin na mchumba wake wakati ambapo Benjamin anamfumania usiku wa manane akiwa mjini kando ya barabara.

28. Benjamin : Kwa nini uko hapa?

Neema : Niko kazini.

Benjamini : Unajiuza? Huoni kwamba unahatarisha maisha yako? Au unataka kuniua mimi?

Neema : Nikuue? Nikuue mara ngapi? Kama ni UKIMWI, tayari unao...mimi mwenzio nina tiketi ya kifo na ninasikitika tu sina pesa, ningekusaidia angalau ya sanda.

Hali hii inatokea baada ya Benjamin kumfumania Neema usiku akifanya biashara ya ukhaba. Kauli ya Benjamin ya kutaka kufahamu alichokuwa anafanya mchumba wake mjini wakati kama ule ni kauli inayodhihirisha kwamba Benjamin anaingilia faragha ya mchumba wake. Hivyo basi, anahasiri uso hasi wa Neema hasa matamano ya uso hasi wa binadamu ya kutaka kufanya chochote anachotaka bila kuulizwa jambo lolote.

3.9 Matumizi ya Kejeli

Kwa mujibu wa Culpeper (1996) matumizi ya kejeli katika mazungumzo ni kitendo kinachohasiri uso. Msemaji anaweza kutumia kejeli kuwasilisha hisia ambazo ni kinyume cha hali halisi ya hisia zake za ndani. Mkakati huu hasa huhusisha msemaji kutumia mikaki ya upole lakini katika hali ambazo hajadhamiria kuonyesha upole wowote kwa msikilizaji.

Matumizi ya kejeli katika filamu husika yanajitokeza katika hali mbalimbali. Kwa mfano, katika filamu ya *Hila* mazungumzo kati ya dada yake Dotinata na Mzee Majuto ni dhihirisho kwamba dada yake Dotinata anamkejili Mzee Majuto kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

29. Dada yake Dotinata : Nakuonea huruma sana shemeji yangu...mke wako anafanya mambo ya ajabu huko nje...jamani mke wako anatia aibu..

Mzee majuto : Mke wangu mimi?

Katika mfano huu, dada yake Dotinata anamwambia Mzee Majuto kwamba anamwonea huruma ilhali katika hali halisi, ana nia ya kutibua ndoa ya dada yake na hana nia ya kuonyesha upole wowote kwa Mzee Majuto. Hivyo basi hisia zake za kuonyesha upole kwa Mzee Majuto si halisi. Mazungumzo haya yanatokea wakati ambapo dada yake Dotinata anaenda kumtembelea shemeji yake Mzee Majuto huku akiwa na lengo la kuvunja ndoa ya Dotinata,

Mfano mwingine unajitokeza katika filamu ya *Upepo wa Baridi* katika mazungumzo kati ya Doris na Batuli wakati ambapo Daniel anapata ajali ya barabarani na hivyo basi Doris anaamua kumjulisha dada yake, kama inavyodhihirika katika mfano huu:

30. Doris : Mume wangu amepata ajali...

Batuli : Kwa hiyo?

Doris : Nimekupigia nikupe taarifa

Batuli : Asante kwa kunipa taarifa.

Katika mfano huu, Batuli anamwambia Doris kwamba anashukuru kwa kupewa taarifa kuhusu ajali ya Daniel lakini katika hali halisi hajakusudia kuonyesha upole wowote kwa dada yake anapomwambia kwamba ameshukuru kwa kupata tarifa hiyo kwa sababu kauli yake ya kwanza kwa Doris inaonyesha kwamba hakuwa na haja ya kuzungumza na Doris. Isitoshe, katika hali hii, angepaswa kumwonea huruma Doris kwa sababu mume wake alikuwa amepatwa na ajali, badala yake anamkejeli.

3.10 Kutowasilisha Chochote

Kwa mujibu wa Culpeper (2005) matumizi ya mkakati wa kutowasilisha chochote hujitokeza katika hali ambapo msikilizaji huwa kimya wakati ambapo anatakiwa kujibu salamu au kutosema asante anapopewa zawadi au kufanyiwa jambo fulani. Matumizi ya mkakati wa kutowasilisha chochote hasa kutojibu salamu na kutoshukuru yanajitokeza katika filamu hizi katika hali mbalimbali japo mkakati huu haujatumiwa sana na waigizaji wa filamu husika.

3.10.1 Kutojibu Salamu

Hali ya kutojibu salamu inajitokeza katika filamu ya *Hila* wakati ambapo Mima na Tabitha wanakimya, Tarzan anapowasalimia. Tarzan anatarajia kwamba Mima na Tabitha watajibu salamu zake badala yake wanakuwa kimya.

31. Tarzan : Habari zenu warembo?

Mima na Tabitha: (kimya)

Mazungumzo haya yanatokea wakati ambapo Tarzan anajumuika na Mima na Tabitha katika mkahawa fulani. Tarzan anapowaslimu, wanakuwa kimya kwa kuwa hawataki kuanzisha mazungumzo yoyote na Tarzan.

Mfano mwingine wa kutojibu salamu unadhihirika katika filamu ya *Tabasamu Ghushi* katika hali ambapo Bosco anakuwa kimya anaposalimiwa na Betha.

32. Betha: Mambo?

Bosco : (Kimya)

Hali hii inatokea wakati ambapo Bosco anamtembelea mchumba wake Batuli nyumbani kwake na badala yake anakaribishwa na Betha ambaye ni dada yake Batuli. Tabia na vitendo vya Betha vya kumkumbatia na kumpiga busu bila kuzingatia kwamba Bosco ni mchumba wa Batuli, vinachukiza Bosco kiasi kwamba anakataa kujibu salamu za Betha.

3.10.2 Kutoshukuru

Hali hii inadhihirika katika filamu ya *Tabasamu Ghushi* wakati ambapo Bosco amemnunulia Batuli zawadi. Katika hali ya kawaida, Batuli anapaswa kusema asante, badala yake anauliza Bosco amemletea nini. Kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

33. Batuli : (Baada ya kupokea zawadi) Umeniletea nini?

Bosco : Njiwa ni wako mwenyewe, manati wamshikia nini?

Mtu anaponunuliwa zawadi, kawaida aliyenunua zawadi hutarajia kwamba anayepokea zawadi atatoa shukrani. Anayepokea zawadi anapokosa kushukuru baada ya kupokea zawadi hudhihirisha utoupole. Hivyo basi ni ada ya anayepokea zawadi au kufanyiwa jambo fulani linalomfaidi kushukuru. Katika mfano huu, kitendo cha Batuli cha kutoshukuru anapopewa zawadi ni dhihirisho la utoupole katika mazungumzo husika.

Mfano mwingine unadhihirika katika mazungumzo kati ya Batuli na Betha wakati ambapo mama yao anaamua kupika vitumbua auze ili apate hela za kukimu mahitaji ya nyumbani. Batuli anapompa Betha kitumbua, anakataa kama inavyojitokeza katika mfano huu:

34. Batuli : (Anampa Betha kitumbua)

Betha : Mimi siwezi kula kitumbua...bora ingekuwa *burger*.

Katika mfano huu, Betha anakosa kushukuru Batuli anapompa kitumbua badala yake anasema kwamba hawezi kula kitumbua kwa sababu baba yake ni tajiri sana, hivyo vyakula anavyokula ni vya gharama ya juu. Katika hali ya kawaida, Betha anapaswa kushukuru Batuli kwa kitendo chake cha ukarimu lakini kauli yake inaonyesha utoupole katika mazungumzo kwa kukosa kushukuru na kukataa kuchukua kile kitumbua.

Betha na Batuli ni madada waliozaliwa na mama mmoja lakini baba tofauti. Baba yake Batuli aliaga dunia Batuli alipokuwa mchanga na hivyo basi hakupata mapenzi ya baba. Baba yake Betha kwa upande mwingine ni tajiri ambaye anashughulikia mahitaji ya Betha kwa kuhakikisha kwamba hakosi chochote huku Batuli na mama yake wakipuuzwa. Betha anapokataa kula kitumbua anachopewa na Batuli, ni dhihirisho kwamba anawadharau kwa sababu ya hali yao ya umaskini.

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kubainisha na kujadili mikakati ya utoupole katika mazungumzo ya waigizaji wa filamu husika. Baada ya kubainisha na kujadili mikakati ya utoupole katika filamu husika kwa msingi wa nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996), jedwali lifuatalo linaonyesha frikwensi ya matumizi ya mikakati mbalimbali ya utoupole inayodhihirika katika filamu husika.

Jedwali 1: Frikwensi ya Matumizi ya Mikakati ya Utoupole katika Filamu Husika

Mikakati Filamu	Mkakati ndani ya rekodi	mkakati hasi wa utoupole	Mkakati chanya wa utoupole	Matumizi ya kejeli	Kutowasilisha chochote	
Upepo wa baridi	14	6	6	4	1	
Hila	18	5	8	3	1	
Majuto	8	5	9	5	0	
Tabasamu ghushi	16	7	4	1	3	
Jumla	56	23	27	13	5	124
Asilimia	45.2%	18.5%	21.8%	10.5%	4.0%	

Kutokana na jedwali hili, inadhihirika kwamba matumizi ya mikakati ya utoupole katika filamu husika ni jumla ya frikwensi 124. Kati ya idadi hii, mkakati ndani ya rekondi wa utoupole ulirekodi frikwensi 56 ambayo ni sawa na asilimia 45.2 %, ukifuatiwa na mkakati chanya wa utoupole ambao ulirekodi frikwensi 27 sawa na asilimia 21.8 %, ukifuatiwa na mkakati hasi wa utoupole ambao ulirekodi frikwensi 23 sawa na asilimia 18.5 %. Mkakati wa

matumizi ya kejeli ulirekodi frikwensi 13 ambayo ni sawa na asilimia 10.5% ukifuatiwa na mkakati wa kutowasilisha chochote ambao ulirekodi frikwensi 5 sawa na asilimia 4.0%.

Ni bayana kwamba mkakati ndani ya rekodi wa utoupole ndio mkakati maarufu zaidi ambao unatumiwa na waigizaji wa filamu husika kudhihirisha utoupole katika mazungumzo. Inabainika kwamba, mkakati ndani ya rekodi wa utoupole unatumiwa zaidi na waigizaji wa filamu ya *Hila* ambayo ilirekodi frikwensi 18, ikifuatiwa na filamu ya *Tabasamu Ghushi* ambayo ilirekodi frikwensi ya 16, ikifuatiwa na filamu ya *Upepo wa Baridi* ambayo ilirekodi frikwensi 14. Mkakati huu hautumiwi sana na waigizaji wa filamu ya *Majuto* ambayo imerekodi frikwensi 8.

3.6 Hitimisho

Katika sehemu hii, kauli za waigizaji wa filamu husika ambazo zinaonyesha utoupole katika mawasiliano zimeainishwa katika mikakati mbalimbali ya utoupole kwa msingi wa nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996). Baada ya kubainisha mikakati mbalimbali ya utoupole inayojitokeza katika filamu husika, matumizi ya mikakati husika imejadiliwa na kutolewa mifano mwafaka kutoka kwa filamu husika. Vilevile, jedwali linaloonyesha frikwensi ya matumizi ya mikakati mbalimbali ya utoupole katika filamu husika linaonyesha kwamba mkakati ndani ya rekodi wa utoupole ndio mkakati unaotumiwa zaidi na waigizaji wa filamu husika huku ukirekodi frikwensi ya 56.

SURA YA NNE

NAMNA YA KUKABILIANA NA HALI YA UTOUPOLE

4.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa Culpeper (2003) msikilizaji anapokumbwa na hali ya utoupole katika mawasiliano, kuna mbinu ambazo anaweza kutumia ili kukabiliana na hali hii. Mbinu hizo ni: Kukubali vitendo vinavyohasiri uso, kukabili vitendo vinavyohasiri uso na kuwa kimya. Msikilizaji anaweza kukabiliana na vitendo vinavyohasiri uso kwa namna ya kumshambulia msemaji au kwa namna ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso.

Katika sura hii, namna mbalimbali za kukabiliana na vitendo vinavyohasiri uso zitajadiliwa na kutolewa mifano kutoka kwa filamu husika. Vilevile, jedwali linaloonyesha frikwensi ya matumizi ya mbinu za kukabiliana na vitendo vinavyohasiri uso litatumika ili kubaini ni mbinu gani inatumiwa zaidi na waigizaji wa filamu husika.

4.2 Kukubali Vitendo Vinavyohasiri Uso

Bousfield (2008) anaeleza kwamba msikilizaji hukubali kitendo kinachohasiri uso kutoka kwa msemaji wakati ambapo anakubaliana na kauli za msemaji ambazo zinadhihirisha utoupole katika mazungumzo. Msikilizaji anapokabiliwa na hali hii, huomba msamaha hata katika hali ambazo hajafanya kosa lolote. Katika filamu husika ambazo zimefanyiwa uchunguzi, mbinu ya msikilizaji kukubali kitendo kinachohasiri uso haijatumikiwa na waigizaji wa filamu husika ili kukabiliana na utoupole katika mawasiliano. Hata hivyo, mbinu ya kuwa kimya, mbinu ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso na mbinu ya kumshambulia msemaji zimetumiwa na waigizaji husika katika kukabiliana na utoupole katika mawasiliano.

4.3 Kukabili Vitendo Vinavyohasiri Uso

Msikilizaji anapokabili vitendo vinavyohasiri uso wake, hakubaliani na kauli za msemaji zinazoashiria utoupole katika mawasiliano wala kuwa kimya. Msikilizaji hukabili hali hii kwa kutenda vitendo vinavyohasiri uso wa msemaji au hujaribu kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso wake kutoka kwa msemaji.

4.3.1 Kukabili Vitendo Vinavyohasiri Uso kwa Namna ya Kujikinga

Msikilizaji hukabiliana na vitendo vinavyohasiri uso kwa namna ya kujikinga kwa kujibu maswali ambayo ameulizwa na msemaji au kwa kumwelezea msemaji mambo ambayo hunuia kuleta maelewano kati ya msemaji na msikilizaji au hata kutoa kauli za kumtania msemaji. Hali hii inajitokeza katika filamu ya *Tabasamu Ghushi* kama inavyobainika katika mfano huu:

35. Bosco : Wewe Betha, kwa nini unakuwa mapepe mapepe hujatulia kiasi hicho? Kwa nini usiige mfano wa dada yako Batuli?

Betha : Sikiliza nikwambie Bosco, usihadaike na uzuri wa rangi, utamu wa chai ni sukari.

Katika mfano, Bosco anatomia mkakati ndani ya rekodi wa utoupole katika mazungumzo kati yake na Betha kwa kumwambia Betha kwamba huwa hajatulia hata kidogo na hiyo si tabia njema. Anazidi kumwambia kwamba aige tabia ya dada yake Batuli. Betha anakabiliana na hali hii ya utoupole kwa kumwelezea Bosco kwamba asihadaike na uzuri wa rangi, utamu wa chai ni sukari. Kwa kutumia msemaji huu katika mazungumzo haya, Betha anajaribu kumwambia Bosco kwamba, si vizuri kumhukumu kwa sababu ya tabia yake anayoiona kwa nje tu, bali anapaswa kumhukumu kwa matendo yake halisi. Isitoshe, anamweleza Bosco kwamba, si vyema kumwamini Batuli sana kwa sababu hajui tabia yake halisi.

Mfano mwigine wa kukabili vitendo vinavyohasiri uso kwa namna ya kujikinga unadhihirika katika filamu ya *Upepo wa Baridi* katika mazungumzo kati ya Doris na Daniel kama inavyojitokeza katika mfano huu:

36. Doris : Unanipiga mimi? Shetani mkubwa wewe! Naondoka, nakuacha na huo ulemavu wako.

Daniel : Usifanye hivyo. Naomba usiondoke. Njoo tuongee mke wangu...

Katika mfano huu, Doris anatumia mkakati chanya utoupole katika mazungumzo kati yake na mume wake, hasa kwa kutumia lugha ya matusi kwa kumwita Daniel shetani mkubwa. Katika hali hii, Daniel anajaribu kumrai mke wake asimwache pekee yake katika hali yake ya ulemavu. Anajaribu kuelezea mke wake kwamba ni bora wakae chini wazungumze ili waweze kupatana. Mazungumzo haya yanatokea wakati ambapo Daniel anakerwa na tabia ya Doris ya kuwa na uhusiano na mwajiri wake. Daniel anapompiga Doris, anaamua kuodoka nyumbani kwake na kwenda kuishi kwa hoteli na mwajiri wake huku akimwacha mume wake katika hali yake ya ulemavu.

4.3.2 Kukabili Vitendo Vinavyohasiri Uso kwa Namna ya Kumshambulia Msemaji

Katika mbinu hii, msemaji anapotenda kitendo kinachohasiri uso wa msikilizaji, msikilizaji hutenda kitendo kinachohasiri uso wa msemaji. Hali hii inapotokea, mara nyingi husababisha ugomvi mkali kati ya wahusika. Kwa mfano, msemaji anapoongea kwa namna ya kumfokea msikilizaji, basi msikilizaji hukabili hali hii kwa kumfokea msemaji. Hali hii inadhihirika katika filamu ya *Majuto* kama inavyobainika katika mazungumzo kati ya Irine na Rita.

37. Rita : Umetoka wapi sasa hivi?

Irine : Nimetoka wapi nikujibu wewe kama nani?

Katika mfano huu, Rita anatumia mkakati hasi wa utoupole hasa mbinu ya kuingilia faragha ya msikilizaji kwa kumuuliza Irine mahali ametoka kwa ukali. Katika mfano huu, Rita anahasiri uso hasi wa Irine hasa matamania ya uso hasi wa binadamu kufanya analotaka bila kuulizwa chochote. Kwa kuwa Irine ni mkubwa kiumri kwa Rita, anamjibu kwa kutenda kitendo kinachohasiri uso chanya wa Rita hasa matamania ya uso chanya wa binadamu ya kutaka kushirikishwa. Kauli ya Irine kwa Rita inadhihirisha namna Irine anamdharau dada yake mdogo. Mazungumzo haya yanotokea wakati ambapo Irine anaenda kumtembelea mchumba wake na kurudi asubuhi yake. Rita anapotaka kufahamu anakotoka Irine, ugomvi mkali unazuka kati yao.

Mfano mwingine unadhihirika katika filamu ya *Upepo wa Baridi* kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya kati ya Rachel na Doris.

38. Rachel: ...nakujua vizuri...tulia na kiwete wako, siyo kudadia mabwana za watu.

Utaumia.

Doris: Mshenzi mkubwa wewe.

Katika mfano huu, Rachel anatumia mkakati ndani ya rekodi wa utoupole kwa kumwamrisha Doris avunje uhusiano kati yake na Alex. Doris kwa upande mwingine anatumia mkakati chanya wa utoupole kwa kumtusi Rachel kwamba ni mshenzi. Mazungumzo haya yanafanyika ofisini kwa Alex wakati ambapo Rachel anagundua kwamba Doris ana uhusiano na mchumba wake na hivyo basi anaamua kulipiza kisasi kwa mchumba wake kwa sababu ya usaliti huu.

4.4 Kuwa Kimya

Kwa mujibu wa Bousfied (2008) msikilizaji anapokabiliwa na hali ya utoupole katika mawasiliano, anaweza kuwa kimya. Kuna sababu tatu kuu ambazo hupelekea msikilizaji kuwa kimya anapokabiliwa na hali ya utoupole katika mawasiliano. Sababu moja kuu ya msikilizaji kuwa kimya ni kwamba, msikilizaji huwa kimya kwa hiari yake mwenyewe. Msikilizaji anapohiari kuwa kimya, aidha hataki kusababisha ubishi mkali kati yake na msemaji au msemaji ana mamlaka zaidi kuliko msikilizaji.

Sababu ya pili ya msikilizaji kuwa kimya ni kwamba, msemaji hampi msikilizaji nafasi ya kutoa maoni yake. Sababu ya tatu ni kwamba, msikilizaji huwa haelewi kauli za msemaji. Mbinu hii ya msikilizaji kuwa kimya anapokabiliwa na hali ya utoupole katika mazungumzo inadhihirika katika filamu husika hasa katika filamu ya *Upepo wa Baridi* kama inavyojitokeza katika mfano huu.

39. Doris : ...sijui nikutupe wapi mbwa wewe.

Daniel : (Kimya)

Katika mfano huu, Doris anatumia mkakati chanya wa utoupole kwa kumtusi Daniel. Kitendo cha Doris cha kumwita Daniel mbwa kinahasiri uso chanya wa Daniel hasa matamano ya uso chanya wa binadamu ya kutaka kukubalika jinsi alivyo. Kwa kuwa Daniel amelemaa miguu na Doris ana nguvu kumlika, basi Daniel anakabiliana na hali hii kwa kuwa kimya. Hali hii inatokea wakati ambapo Daniel hawezi kukimu mahitaji ya mke wake, hivyo basi Doris anapomwambia kwamba anahitaji hela ili ashughulikie mahitaji ya nyumbani, Daniel anamweleza kwamba hana pesa lakina ataomba msaada. Doris anakasirika na mume wake na kutoa kauli zinazohasiri uso chanya wa Daniel.

Mfano mwingine unadhihirika katika filamu ya *Tabasamu Ghushi* kama inavyojitokeza katika mazungumzo kati ya Kagomba na Grace.

40. Kagomba : Nikuvumilie? ...utakapoona sura yangu, nikute vitu viko nje au kodi yangu...

Grace : (Kimya)

Katika mfano huu, Kagomba anatumia mkakati ndani ya rekodi wa utoupole kwa kuamrisha Grace alipe kodi ya nyumba au ahame. Grace anakabiliana na hali hii kwa kuhiari kuwa kimya kwa sababu Kagomba ana mamlaka zaidi kumliko na hivyo basi hataki kutoa kauli ambazo zinaweza kuzua ugomvi kati yake na Mzee Kangomba.

Mfano mwingine unadhihirika katika filamu ya *Upepo wa Baridi* kama inavyojitokeza katika mazungumzo kati ya Doris na Rachel wakati ambapo Doris anarejea kazini baada ya likizo kama inavyojitokeza katika kauli hii:

41. Doris : Ati wewe ndiye mhusika wa hapa?

Rachel : (Kimya)

Katika mfano huu, Doris anatumia mkakati wa matumizi ya kejeli kuonyesha utoupole katika mazungumzo kati yake na Rachel. Hali hii inatokea baada ya Alex kumwajiri Rachel kazi ambayo Doris alikuwa anafanya kabla ya mume wake kupata ajali na kulemaa. Anaporudi kazini baada ya kuhudumia mume wake, anakuta kwamba nafasi yake ya kazi ofisini kwa Alex imechukuliwa na Rachel. Rachel anakabiliana na hali hii ya utoupole kwa kuwa kimya kwa sababu hataki kuzua hali ya ugomvi mkali kati yake na Doris.

Jedwali lifuatalo linaonyesha frikwensi ya matumizi ya mbinu za kukabiliana na utoupole katika mikakati husika ya utoupole kwenye filamu nne husika.

Jedwali 2: Frikwensi ya Matumizi ya Mbinu za Kukabiliana na Utoupole Katika Filamu Husika.

	Kuwa kimya	Kujikinga	Kushambulia msemaji	Kukubali vitendo vinavyohasiri uso	
Mkakati ndani ya rekodi	10	38	8	0	
Mkakati chanya	5	15	6	0	
Mkakati hasi	5	14	5	0	
Matumizi ya kejeli	4	6	3	0	
Kutowasilisha chochote	3	2	1	0	
Jumla	27	75	23	0	125
Asilimia	21.6	60	18.4	0	

Katika jedwali hili, imebainika kwamba mbinu ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso ndiyo inatumiwa zaidi na waigizaji wa filamu husika ili kukabiliana na hali za utoupole kwa kurekodi frikwensi ya 75 sawa na 60% ikifuatiwa na mbinu ya kuwa kimya ambayo ilirekodi frikwensi ya 27 sawa 21.6 %.

Mbinu ya kuwa kimya ilifuatiwa na mbinu ya kumshambulia msemaji ambayo ilirekodi frikwensi ya 23 sawa na 18.4 %. Vilevile, imebainika kwamba matumizi ya mbinu ya kukubali vitendo vinavyohasiri uso haitumiwi na waigizaji wa filamu husika ili kukabiliana na hali ya utoupole katika mazungumzo. Matumizi ya mbinu ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso inatumika zaidi katika mkakati ndani ya rekodi wa utoupole ambapo ilirekodi fwekwensi ya 38 na matumizi ya mbinu hii ilirekodi frikwensi ya chini katika mkakati wa kutowasilisha chochote ambapo kuna frikwensi ya 2. Mbinu ya kuwa kimya ilirekodi frikwensi ya 10 katika mkakati ndani ya rekodi, huku mbinu hii ikirekodi frikwensi ya 3 katika mkakati wa kutowasilisha chochote.

Katika jedwali hili, ni bayana kwamba mbinu ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso ndiyo hutumiwa zaidi na waigizaji wa filamu husika katika kukabiliana na hali ya utoupole katika mawasiliano ikifuatiwa na mbinu ya kumshambulia msemaji. Mbinu ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso inatumika zaidi katika mkakati ndani ya rekodi wa utoupole kwa sababu huu ndio mkakati unaotumiwa zaidi na waigizaji wa filamu husika kudhihirisha utoupole katika mawasiliano. Mbinu hii pia inatumika zaidi na wahusika wa filamu husika ili kuendeleza mazungumzo kati ya waigizaji wa filamu husika kinyume na mbinu ya kumshambulia msemaji ambayo ilirekodi frikwensi 23 sawa na 18.4 % ambayo husababisha ubishi mkali kati ya msemaji na msikilizaji hali ambayo hupelekea kuvunjika kwa mawasiliano.

4.5 Hitimisho

Katika sehemu hii, mbinu za kukabiliana na utoupole zinazotumiwa na waigizaji wa filamu husika zimejadiliwa na kutolewa mifano mwafaka kutoka kwa filamu zilizoteuliwa kufanyiwa uchunguzi. Jedwali linaloonyesha frikwensi ya matumizi ya mbinu za kukabiliana na hali ya utoupole na waigizaji wa filamu husika limebainisha kwamba mbinu ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso ndiyo inatumiwa zaidi kukabili hali ya utoupole huku ikirekodi frikwensi ya 75 sawa na 60 % huku mbinu ya kukubali vitendo vinavyohasiri uso haitumiwi na waigizaji wa filamu husika kwa sababu wasikilizaji wanapokabiliana na hali ya utoupole kutoka kwa wasemaji, hawakubaliani na kauli zao. Pia imebainika kwamba ugomvi kati ya msemaji na msikilizaji hutokea kutokana na namna ambavyo msikilizaji anakabiliana na hali hii.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii, matokeo ya uchunguzi yatajadiliwa na kuthamini kama malengo ya utafiti yameafikiwa au la, na kutoa mapendekezo kuhusu tafiti zingine zinazofaa kufanywa kuhusu suala la utoupole katika mawasiliano.

5.2 Kutathmini Ufanisi wa Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yalikuwa:

1. Kubainisha na kujadili mikakati ya utoupole katika mazungumzo ya waigizaji wa filamu husika.
2. Kujadili namna waigizaji wa filamu husika wanavyokabiliana na hali za utoupole katika mawasiliano.

Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kwamba mikakati ya utoupole iliyopendekezwa na Culpeper (1996) inatumiwa na waigizaji wa filamu za *Hila*, *Tabasamu Ghushi*, *Upepo wa Baridi* na *Majuto* kudhihirisha utoupole katika mchakato mzima wa mawasiliano. Imebainika kwamba mkakati ndani ya rekodi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole, matumizi ya kejeli na mkakati wa kutowasilisha chochote ndiyo mikakati ya utoupole inayotumiwa na waigizaji wa filamu husika.

Pia imebainika kwamba mkakati ndani ya rekodi wa utoupole ndio unaotumiwa zaidi na waigizaji wa filamu husika kwa kurekodi frikwensi ya 56 sawa na 45.2 %. Mkakati wa kutowasilisha chochote ndio mkakati wa utoupole ambao hautumiwi sana kwa kurekodi frikwensi ya 5 sawa na 4.0 %.

Katika kujadili mikakati ya utoupole inayotumika katika kauli za waigizaji wa filamu husika, imebainika kwamba kuna sababu ambazo huchangia wasemaji kutumia mikakati ya utoupole katika mawasiliano. Sababu kuu inayojitokeza katika filamu husika ni kwamba tofauti za kimamlaka kati ya waigizaji huchangia pakubwa katika matumizi ya mikakati ya utoupole. Tofauti hizi za kimamlaka zinabainika katika nguvu za mwili za wahusika, nguvu za uchumi za wahusika au mamlaka ya mhusika katika familia au jamii.

Katika kujadili namna waigizaji wa filamu husika wanavyokabiliana na hali za utoupole katika mawasiliano, matokeo ya utafiti huu yamebainisha kwamba mbinu ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso ndiyo mbinu inayotumiwa zaidi na waigizaji wa filamu husika kwa kurekodi frikwensi ya 75 sawa na 60 % , huku mbinu ya kukubali vitendo vinavyotishia uso haitumiwi na waigizaji wa filamu husika kukabili hali za utoupole katika mazungumzo.

Hivyo basi, waigizaji wa filamu husika wanapokabiliwa na hali za utoupole hufanya juhudi za kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso ili kuepuka kuzua ugomvi kati ya msemaji na msikilizaji. Vilevile, uso ni kitu dhaifu kama wanavyoeleza Brown na Levinson (1987) kwamba katika mawasiliano uso unaweza ukahasiwa au kuumbuliwa, na hivyo basi sharti msemaji ahakikishe kwamba anahifadhi siyo tu uso wa msikilizaji bali pia uso wake.

5.3 Changamoto za Utafiti

Changamoto iliyokumba utafiti huu ni ugumu wa kupata filamu ambazo zingetupa data mwafaka ili kufanikisha uchunguzi husika. Baadhi ya filamu za Tanzania ambazo tulizitoa kwenye mtandao wa YouTube zilikuwa na sauti hafifu na zingine miziki inayotumiwa katika filamu ilikuwa na sauti ya juu kuliko sauti ya waigizaji. Hata hivyo, baada ya kudadisi zaidi, tulifanikiwa kupata filamu ambazo sauti ya waigizaji inasikiki kwa urahisi.

5.4 Mapendekezo

Mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe kuhusu matumizi ya mikakati ya utoupole katika tanzu zingine za fasihi kama vile riwaya, tamthilia na vipindi vya burudani vya runinga ili kubainisha namna matumizi ya mikakati ya utoupole yanaendeleza maudhui au kuwanjenga wahusika au namna matumizi ya mikakati ya utoupole hujenga fani katika tanzu za fasihi.

Utafiti huu umeshughulikia filamu nne pekee kutoka nchini Tanzania, mtafiti anapendekeza utafiti mwingine ufanywe ili kushughulikia suala la matumizi ya mikakati ya utopole katika filamu za Kiswahili nchini Kenya au filamu nyingine kutoka nchini Tanzania ili kubainisha kama mikakati inayotumika katika filamu zilizofanyiwa uchunguzi ni sawa na mikakati inayotumika katika filamu zingine.

Mtafiti pia anapendekeza uchunguzi mwingine ufanywe kuhusu namna ambavyo suala la utoupole katika filamu linazua ucheshi katika filamu mbalimbali. Kimsingi, katika mazungumzo, kauli za msemaji zinazodhihirisha utoupole huzua ucheshi kwa wasikilizaji na watazamaji wao. Hivyo basi, mtafiti anapendekeza utafiti mwingine ufanywe kuhusu majukumu ya utoupole katika filamu.

MAREJELEO

- Bousfield, D. na Miriam, L. (2008). *Impoliteness in Language*. Berlin: Mouton de Gruyter.
- Bousfield, D. (2008). *Impoliteness in Interaction*. Philadelphia: John Benjamin Publishing Company.
- Budi, W. (2015). “*Impoliteness Used in Action Movies*.” Muhammadiyah University of Surakarta.
- Brown, P. & Levinson, S. (1987). *Politeness: Some Universals in Language Usage*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Culpeper, J. (1996). Towards an Anatomy of Impoliteness. *Journal of Pragmatics* 25: 349-367
- Culpeper, J. (2001). *Impoliteness: Using Language to Cause Offence*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Culpeper, J., Derek, B., and Anne, W. (2003). Impoliteness Revisited with Special Reference to Dynamic and Prosodic Aspects. <http://id.scribd.com/doc/20554112/Culpeper-Impoliteness-Revisited>. Retrieved on December 2, 2016.
- Culpeper, J. (2005). Impoliteness and Entertainment in the Television Quiz Show: The weakest link. *Journal of Politeness Research* 1: 35-72.
- Eelen, G. (2001). *A Critique of Politeness Theories*. Manchester: St Jerome.
- Fraser, B. & Nolen, W. (1981). The Association of Deference with Linguistic Form. *International Journal of the Sociology of Language* 27:93-109.
- Goffman, E. (1967). *Interaction Ritual*. Chicago: Aldine Publishing.

- Goro, M. (2014). “*An Analysis of Impolite Language used by Matatu Conductors: A case Study of Matatus Plying Route 32 From Nairobi City Centre to Dandora.*” Tasnifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Grice, H.P. (1975). *Logic and Conversation*. New York: New York Academic Press.
- Kinyua, G. W. (2015). “*Ukiukaji wa Kanuni za Upole katika Mhanga Nafsi Yangu.*” Tasnifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Lachenict, L. (1980). *Aggravating Language: A Study of Abusive and Insulting Language. International Journal of Human Communication 13: 607-688.*
- Lakoff, R. (1973). *The Logic of Politeness: Or Minding your P’s and Q’s. Chicago Linguistic Society pp 292-305.*
- Leech, G. (1983). *Principles of Pragmatics*. London: Longman.
- Massamba et al (2004). *Fonolojia ya Kiswahili sanifu (FOKISA) Sekondari na Vyu*. Dar-es-Salaam: TUKI.
- Mills, S. (2003). *Gender and Politeness*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Mponguliana, J. A. J. 1982. “*The Development of Film in Tanzania.*” Tasnifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Dar- es- Salaam.
- Nabelle, P. (2015). “*A Pragmatic Analysis of impoliteness Strategies used in Paranorman Movie.*” Unpublished Thesis: Yogyakarta State University.
- Njewe, D.C. (2007). “*Manifestation of Cultural performances in Traditional African Films.*” Tasnifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Dar-es- Salaam.
- Pembe, H. (2015). “*Mikakati ya Tafsiri na usawa Wa Ujumbe katika Tafsiri ya Mazungumzo ya Kingereza kwenye Filamu za Kiswahili Nchini Tanzania.*” Tasnifu ambayo imechapishwa: Chuo Kikuu cha Moi.

Shule, V. (2014). Sanaa kwa Maendeleo Tanzania: Kati ya Kujiweza na Kuwezwa. *Swahili Forum* 21:26-39.

Suwed, A. A. (2013). “*Usawiri wa Ujinsia katika Filamu: Uchunguzi wa Matumizi ya Lugha katika Filamu za Steven Kanumba,*” Tasnifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar-es-Salaam: Educational Publishers and Distributors.

VIAMBATISHO

Kiambatisho I

Data ya filamu ya *Hila*

Dada yake Dotinata: Nakuonea huruma sana shemeji yangu.

Mzee Majuto: Vipi? Mimi sina matatizo.

Dada yake Dotinata: Haya maisha unayoishi, wewe unajua uko sawa lakini hauko sawa. Una mzigo mkubwa sana wa matatizo katika familia yako.

Mzee Majuto: Hapana shemeji. Mimi niko sawa, nina raha na furaha. Niko na mke wangu, nina watoto wangu. Matatizo yametokea wapi tena?

Dada yake Dotinata: Wewe unajua uko sawa lakini hauko sawa. Yaani roho inaniuma. Mke wako anavyokufanyia huko nje!

Mzee Majuto: Mke wangu mimi?

Dada yake Dotinata: Anakusaliti. Anatoka nje ya ndoa yake. Anafanya mambo ya ajabu huko nje, nikikwambia huwezi kuamini.

Mzee Majuto: Hapana shemeji. Shemeji, kwani mna ugomvi wewe na dada yako?

Dada yake Dotinata: Dotinata ana wanaume nje, anafanya gharama kwa hao wanaume wa nje mpaka kwa familia zao. Na huyu mtoto wa kiume siyo wako. Hebu mwenyewe mwangalie vizuri. Kwani katika familia yenu kuna chotara nyinyi? Basi huyu mtoto si wako, na baba yake mimi namjua mpaka namba ya simu nitakupatia. Anakuzunguka mwenzio. Jamani mke wako anatia aibu huko nje. Kinyaa.

Dotinata: Vipi? Una nini leo?

Mzee Majuto: Usinishike! Niache!

Dotinata: Una nini mume wangu?

Mzee Majuto: Hivi unasikia ninavyosema au husikii? Umetoka wapi saa hizi?

Dotinata: Kwani sikuwa nimekwenda kwenye shughuli zangu mume wangu?

Mzee Majuto: Kumbe una kingine unachokifanya kwingine?

Dotinata: Kama kawaida unajua mimi nikitoka hapa naenda kwenye kazi zangu.

Mzee Majuto: Unakotoka ndiko uliko niambia? Umetoka kwingine na nina uhakika.

Unavunja kabisa hadhi na heshima ya ndoa. Nini maana yake?

Dotinata: Nimekufanyia kitu gani mume wangu?

Mzee Majuto: Kwa taarifa yako, unayoyafanya kila siku, yote nimeyapata leo.

Dotinata: Si kila binadamu anapenda jinsi tunavyoishi. Huyu ni shetani kaja kuvuruga ndoa yangu.

Mzee Majuto: Mimi sikuhitaji kabisa.

Dotinata: Mume wangu, kweli kabisa sijawahi kukuendea kinyume na haitowezezana hata siku moja. Jaribu kuchunguza kwanza. Mbona unaamini maneno ya kuambiwa haraka?

Mzee Majuto: Mambo gani unafanya huko nje? Unakwenda kuhonga hela watu...siamini! Ninachotaka mimi, leo wewe na watoto wako, sitaki kuwaona hapa nyumbani. Nimechoka! Nimechoka! Nimechoka! Nimekuwa mnyenyekevu na mvumilivu kwako kumbe unanifanyia vituko vya ajabu. Unanisaliti! Kwa nini ufanye kitu kama hicho?

Datinata: Nichunguze kwanza mume wangu.

Mzee Majuto: Hapana! Sikuhitaji. Kitu unachofanya si kizuri kwangu. Ni kashifa, unanitukanisha. Kumbe natembea natembea huko nje watu wanasema kwamba

mimi ni mume bwege na sina habari? Mimi nataka utoke.

Dotinata: Mume wangu chunguza kwanza haya mambo. Siendi kinyume na sijawahi toka nje ya ndoa mimi. Chunguza, binadamu si wazuri.

Mzee Majuto : Hili suala halina ubishi. Nenda tu, toka uende.

(Siku iliyofuata)

Mzee Majuto: Si nilisema nikija nisiwakute humu ndani? Toka! Toka! Kwa nini hutaki kusikia? Toka nje!

Dotinata: Mume wangu, unataka niondoke na watoto niende wapi?

Mzee Majuto: Hujui pa kwenda? Ngoja nikuonyeshe pa kwenda.

Dotinata: Yaani nimezunguka kutwa nzima jamani hata mchicha wenyewe nimeshindwa kumaliza kuuza. Angalia shoga yangu, mimi hapa nimeuza Tsh. 250. Sijui wanangu nitawapa nini jamani. Mimi shoga yangu nimechoka.

Shoga yake Dotinata: Kama umechoka unataka ufanye nini?

Dotinata: Unisaidie shoga yangu, basi tuuze pamoja. Naona wewe unafanikiwa.

Dada yake Dotinata: Hivi wanangu, mnaridhika na haya maisha? Hivi wewe Tarzan unajua mama yako ana shilingi ngapi kwenye benki?

Tarzan: Hapana sijui.

Angel: Sasa hayo yanatuhusu nini mama mdogo?

Dada yake Dotinata: Yanawahusu nyinyi... kinachoniuma zaidi mpaka leo nawaambia, lakini iwe siri yenu. Mama yenu huko nje, amefungulia watu maduka, anasomesha watu, ana wavulana ambao anawagharamia kwanzia wao wenyewe mpaka familia zao. Nyinyi mmekaa tuu hamna mpango wowote. Hamna lolote mnalolijua.

Tarzan: Unamaanisha nini kusema hivyo?

Dada yake Dotinata: Nina maanisha, mama yenu ana wanaume huko nje, halafu

anawagharamia kwa kila kitu. Anagharamia wanaume mpaka familia zao.

Angel: Mama mdogo hapana, mama hawezi kufanya hivyo. Hilo nakataa.

Dotinata: Wewe utajua wapi? Mama yenu huko nje anaitwa malaya. Anagharamikia huko nje kupita maelezo. Ananuka huko nje hafai.

Angel: Wewe mama mdogo una yako. Mama hawezi kufanya vitu hivyo.

Dada yake Dotinata : Hana lolote, ni mnafiki mkubwa...msiwe wajinga, siku zinakwenda, leo ndiyo siku ya kuhangaika, kesho mtajutia.

Tarzan: Labda mama akija tutaongea naye.

Dada yake Dotinata: Mtaniharibia, tafuteni unga, mtilieneni mama yenu halafu mkafungue

kwenye sefu mtafute chochote mtoke mkaanzishe maisha yenu. Siyo

kukaa hapa kama mzigo wa nyanya.

(Baada ya Dotinata kutoka kazini)

Dotinata: Tarzan mwanangu, uwe makini sana. Wiki mbili tatu hizi naona una mabadiliko

makubwa sana. Sijui kitu gani kinawasibu. Nasikia maneno na mimi

mwenyewe naona mwenendo umebadilika. Angalia sana, si kila anayekuchekea

anakupenda.

Tarzan : Sasa ina maana kwamba mimi ni mtoto mpaka ufuatilie mambo ambayo hayapo?

Hivi wewe umezeeka au vipi?

Dotinata: Kwa hiyo mwanangu ikuwe kama nimezeeka ndiyo nisiwafuatilie wanangu

mnafanya nini?

Tarzan: Potezea hayo.

Dotinata: Unanijibu hivyo mwanangu?

Tarzan: Mimi niko ndani bwana.

Dotinata: Yaani unanijibu hivyo jamani?

(Jikoni)

Tarzan: Hivi wewe, unajipendekeza hivi ili uongezewe mshahara au vipi?

Kijakazi: Nimefanya nini?

Tarzan: Sikiliza nikwambie, iwe mwanzo na mwisho kuingilia familia yetu. Tena ukome.

Siyo kuingilia familia usizozijua. Siyo kuropokwa ovyo maneno.

Dotinata: Tarzan, hiyo tabia umeianza lini?

Tarzan: Anaingilia mambo ambayo hayamhusu.

Dotinata: Yapi? Mwanangu umeanza bangi eeh?

Tarzan: Mama bwana, achana na mimi bwana!

(Uani)

Dotinata: Wewe Tarzan, unataka kufanya nini? Nakuuliza unafanya nini hapo kwenye gari ?

Tarzan: Nataka nitoke nikastarehe.

Dotinata: Toka bila gari.

Tarzan: Mama, mambo mengine siyo ya kufuatilia.

Dotinata: Umerogwa?

Tarzan: Mama unanibania bwana. Hutaki kunipa hata gari moja? Magari haya yote yamekaa

tu hapa.

Dotinata: Wacha yakae.

Tarzan: Sijui vipi wewe...

(Sebuleni)

Dotinata: Tarzan, kwa nini unafanya hivyo? Mwanangu, kwa nini unaamua kunijibu namna ile? Unataka kunipa ugonjwa wa shinikizo la damu? Nikifa utafurahi?

Tarzan: (Kimya)

Dotinata: Unaona anavyofanya kaka yako?

Angel: Sikiliza mama, naomba uniache vivi hivi. Ushanielewa? Wewe kama unataka kuongea na mwanao, ongea naye ndiye huyo. Mimi sitaki kabisa, yaani niache!

Tarzan: Unatupotezea muda tu.

Dotinata: Tarzan mwanangu, mnanipa wakati mgumu wanangu. Kwa nini lakini?

(Ndani ya mkahawa)

Tarzan: Mambo? Habari zenu werembo?

Mima na Tabitha: (Kimya)

Tarzan: Mimi naitwa Tarzan, sijui wenzangu mnaitwa nani?

Tabitha: Eeh! Mambo ya kujuana majina tena vipi? Unataka kutupeleka kwa mganga?

Mima: Nashangaa.

Tarzan: Sina maana hiyo. Nahitaji tu kuketi nanyi.

Tabitha: Hatuhitaji kuketi na mtu mwingine.

Tarzan: Mimi nina gari yangu pale nje.

Mima: Una nini? Gari?

Tarzan: Eeeh...

Mima: Gari kitu gani?

Tabitha: Kaka, tushakwambia hatuhitaji kuketi na wewe. Unaweza ukaenda. Mbona unalazimisha? Tembea huko!

Tarzan: Haya basi, siyo lazima.

(Ndani ya chumba cha mankuli, nyumbani kwao Tarzan)

Angel: Wewe! Liangalie linavyokula. Unajua tu kula humu ndani, hicho tu ndicho unachokiweza. Kula na umbeya. Hivi wewe unajua kwamba unajua sana umbeya? Hivi hujui kwamba mimi na kaka yangu tukiamua uache kazi unaacha kazi muda wowote ule?

Tarzan: Nashangaa

Angel: Wewe yamekushinda kwenu ndiyo maana unafanya kazi za ndani kwetu. Umbeya unauleta wa nini? Wewe si umeshindwa kuishi kwenu? Huko maisha magumu na sura lako lilivyo libaya wala hakuna mwanamume wa kukuo, ndiyo maana umekuja kufanya kazi za ndani hapa. Utaondoka humu ndani. Pumbavu.

Kijakazi: (Kimya)

Kiambatisho II

Data ya filamu ya *Tabasamu Ghushi*

Betha: Batuli nawe, hivi huchoki kusoma? Muda wowote wewe ni kitabu na kalamu.

Huchoki?

Batuli: Betha, huu ni mustakabali wa maisha yangu. Kwa hiyo lazima niweke mkazo.

Betha: Ukweli. Lakini nafikiri hutaki kurudia ile kazi yako ya kuwa *house girl*.

Batuli: Betha mdogo wangu, kazi yoyote ni sehemu ya maisha. Ila kusoma ni wajibu wangu, na hii hainifanyi nijione tofauti na watu wanaofanya kazi za ndani.

Betha: Sawa, lakini sababu kubwa ambayo unayo ya kusoma ni kutorudia hiyo kazi yako.

Betha: (*Kwa mama yake*) Mama wewe kila siku samaki? Haya sasa yanachosha.

Grace: Betha, aliyekulazimisha ule vyakula ambavyo ninanunua ni nani? Si uende kwa baba yako? Baba yako si ana kila kitu? Nenda.

Betha: Kwani nimekataa mama? Kwa baba yangu kila kitu kipo, tatizo kwa baba siko huru. Hamna uhuru kabisa. (*Kwa Batuli*) *Chef chef*, kafanye kazi yako. Nenda basi.

Grace: Betha, kwa nini unakosa heshima wewe? Kwa nini huheshimu dada yako? Mbona uko na dharau kiasi hiki mwanangu?

Betha: (kimya)

Betha: Oyaa! Hicho chakula bado? Batuli, mama, njaa inauma jamani.

Batuli na Grace: (Kimya)

(*Ndani ya chumba cha mankuli*)

Grace: Betha wewe.

Betha: Mmmh, unasema nini?

Grace: Natumaini samaki amekuridhisha, sasa ukishiba, ukusanye vyombo ukaoshe.
Unasikia?

Betha: Nikaoshe? Mimi nikaoshe vyombo? Siwezi kuosha vyombo mama.

Grace: Kazi yako humu ndani wewe ni nini? Mwanangu mwonee huruma dada yako. Yaani wewe kula, kulala na muziki tu ?

Betha: Lakini mama, hayo mambo yamepitwa na wakati. Hayo mambo ni ya zamani. Vyombo mtu yeyote anaweza kuosha. Hata wewe, hata yeye anaweza kuosha. Lazima nioshe mimi? Hata hivyo nimekumbuka kuna house girl mzoefu pale anaweza kutusaidia.

Grace: Haya ni maneno gani unaongea Betha? Mbona unadharau dada yako? Naomba utambue kwamba wewe ni binti wa kitanzania, mtoto wa kiafrika. Unapaswa kufanya kazi za ndani.

Betha: (Kimya)

(Ofisini kwa Nashon)

Nashon: Muda mwingi ninakuuliza unakimya tu. Sijui una tatizo gani?

Grace: Nimefukuzwa shule.

Nashon: Kwa kosa gani?

Grace: Nina ujauzito.

Nashon: Unasema? Una ujauzito? Umeutoa wapi?

Grace: Si wewe Nashon.

Nashon: Mpumbavu wewe. Hivi unafikiri nani wa kulaumiwa? Uliwezaje kupata mimba wakati unajua kwamba wewe ni mwanafunzi? Unategemea nini? Unataka kunipa kesi mimi?

Grace: Nashon, wewe huna sababu ya kunilaumu kwa kitu ambacho tayari kimetokea.
Ingebidi wewe na mimi tukae pamoja tushauriane kitu cha kufanya.

Nashon: Sina muda mchafu wa kukaa na wewe kujadili vitu kama hivyo. Hiyo mimba siji utaipeleka wapi. Tafuta mtu wa kupelekea. Siyo mimi.

Grace: Nashukuru sana ila sikujua raha zote nilizokupa mwisho wake ni wa karaha kunitupa kwa namna hii.

Nashon: Nimesema ondoka! Sitaki mashairi yako Grace. Na huo mlango uwe mwanzo na mwisho wa kuingia humu ndani. Toka!
(Nyumbani kwake Batuli)

Betha : Mambo?

Bosco : (Kimya)

Bosco : Wewe Betha, kwa nini unakuwa mapepe hujatulia kiasi hicho? Hivi hujui kwamba mimi ni shemeji yako? Wewe umekuwa mapepe mapepe tu. Kwa nini usiige mfano wa dada yako Batuli?

Betha : Sikiliza nikwambie Bosco, usihadaike na uzuri wa rangi, utamu wa chai ni sukari.

Bosco : Mbona unaondoka na mizigo si yako?

Betha : Chukuweni basi.

Batuli : (Anampa Betha kitumbua)

Betha : Mimi siwezi kula kitumbua...

(Baba yake Betha anapotembelea Betha nyumbani kwake Grace)

Betha : Umewahi kuona dola wewe? Umezoea vishilingi Ishirini vyako vya vitumbua.

Grace : (Kimya)

Betha : (Anampa Batuli pesa) Chukua! Unaringa huku maskini? Shauri yako, utalala njaa.

Hiyo hela ununue chakula upike. Ninaenda zangu kulala. Halafu, ndani kuna nguo zangu chafu ukirudi unifulie.

Batuli : (Kimya)

(Baba yake Betha anapomfuata Betha akaishi naye)

Grace : Kwa hivyo umeamua kuchukua hayo maamuzi?

Baba Betha : Sikiliza Grace, nimekuwa nikileta matumizi hapa kwa ajili ya kuhudumia binti yangu tu na siyo kuhudumia nyumba ya mayatima.

Grace : Ukiongea hivyo, utakuwa unakosea. Naomba utambue kwamba hawa ni ndugu.

Mbona unapenda kuweka matabaka?

Baba Betha : Hawa ni ndugu? Kama ulitaka wawe ndugu, kwa nini hukuzaa na mwanamume mmoja? Kama kila mmoja hapa ana baba yake, basi ni sawa na nyani kila mmoja kuchunga mke wake.

Grace : (Kimya)

(Nyumbani kwake Grace)

Kagomba : Ninachohitaji ni kodi yangu au unikabidhi nyumba yangu.

Grace : Ninakuelewa lakini si unaona hali yangu si nzuri?

Kagomba : Sasa sihitaji rongo rongo. Hivi kwa nini mnang'ang'ania kuishi mjini msirudi vijijini? Kwani wanaoishi vijijini hawapendi kuishi mjini? Hapa mjini hapendwi mtu, ni pesa .

Grace : Naomba univumilie kidogo tu.

Kagomba : Nikuvumilie? Sasa mimi ndiye Kagomba wa Kagomba. Natoka nitarudi leo hii.

Utakapoona sura yangu, nikute vitu viko nje au kodi yangu. Leo hii, siyo siku nyingine.

Grace : (Kimya)

(Nyumbani kwake Batuli)

Grace : Betha, dada yako kanunuliwa gari.

Betha : Kama hiyo ni gari, sasa mimi yanihusu nini?

Batuli : Betha mdogo wangu, sisi ni familia moja, mbona usinifurahie?

Betha : Mimi nitaendesha gari ambayo nitanunua kwa pesa yangu, siyo gari ya kuhongwa na mabwana.

Batuli : (Kimya)

(Barabarani)

Bosco : Sitafanya baya lolote kwako, ila kitu kimoja ninachohitaji kutoka kwako , achana na mchumba wangu kwanzia leo.

Benjamin: Kaka, naomba unisikilize.

Bosco : Sihitaji kusikiliza chochote kutoka kwako. Unafikiri una nini cha kuniambia mimi?

Na iwapo utasitasita katika hili, sitaona ajabu kuvunja ahadi yangu niliyokupa hapo mwanzo.

Benjamin : Usitembee naye tena.

Bosco : Wewe kijana, rudi huku. Yaani unichukulie mwanamke wangu halafu unipangilie masharti ya kuishi naye? Hujui kwamba nataka kufunga naye ndoa?

Benjamin : Simaanishi hivyo. Kama ningejua yote uliyoniambia kabla, nisingefanya nilichokifanya.

Bosco : Nyinyi vijana akili zenu huwa hazipo ndani ya vichwa vyenu. Zipo ndani ya hizi nywele mnazofuga mnazoita rasta.

Benjamin : Ninajua una uchungu, ninauona, lakini ninachokwambia kina faida kwako wewe mwenyewe. Tafadhali nisikilize.

Bosco : Eeh, ongea.

(Nyumbani kwake Benjamin)

Batuli : Benjamin, ina maana hunioni?

Benjamin : Unashida gani wewe?

Batuli : Naomba kuongea na wewe

Benjamin : Sijisikii kuongea na wewe na wala sina muda .

Batuli : Nimekukosea nini Benjamin?

(Barabarani usiku)

Benjamin: Kwa nini uko hapa?

Neema : Niko kazini.

Benjamin : Unajiuza? Huoni unahatarisha maisha yako? Au unataka kuniua mimi?

Neema : Nikuue? Nikuue mara ngapi? Kama ni UKIMWI, tayari unao. Nakushauri uende ukapime. Mimi mwenzio nina tiketi ya kifo na ninasikitika tu sina pesa, ningekusaidia angalau ya sanda.

Benjamin : (Kimya)

Kiambatisho III

Data ya filamu ya *Upepo wa Baridi*

Doris : (Kwa simu) Shikamoo dada Batuli.

Batuli : Marahaba. Mbona unanipigia simu usiku hivi? Una tatizo gani?

Doris : Mume wangu amepata ajali. Kwa sasa hivi ninavyoongea na wewe, yupo hospitalini.

Hali yake ni mbaya sana.

Batuli : Kwa hiyo?

Doris : Kwa hiyo? Si nimekupigia nikupe taarifa?

Batuli : Eeeh, kumbe ulikuwa unanipa taarifa? Nashukuru kwa kunipa taarifa. Usiku mwema.

Doris: (Kwa simu) Bwana Alex, samahani nilikuwa nataka nikutarifu kuwa leo sitaweza

kufika ofisini, mume wangu amepata matatizo yupo hoi hospitalini.

Alex : Wewe vipi? Ina maana unaacha kazi ya muhimu hapa ofisini ili uende hospitalini?

Doris : Ninakwambia kwamba mume wangu yupo hospitalini amepata ajali unaniambia kuna

kazi ya muhimu?

Alex : Hapana, siyo hivyo. Utanijulisha yatakapokuwa yamekwisha.

(Ofisini kwa Alex)

Doris : Habari yako?

Rachel : Salama, nikusaidie nini?

Doris : Unasema unisaidie?

Rachel : Nakuuliza nikusaidie nini kwa sababu mimi ndiye mhusika hapa?

Doris : Eti wewe ndiye mhusika wa hapa?

Rachel : (Kimya)

Alex: Vipi hali ya mume wako?

Doris : Inasikitisha sana, mume wangu amepata kilema cha maisha.

Alex : Amelemaa kivipi?

Doris : Miguu yote haifanyi kazi.

Alex : Sawa. Nasikitika kukwambia kwamba nafasi yako kwa sasa ina mtu.

Doris : Ina maana hukujali matatizo yangu?

Alex : Nilikwambia kuna kazi ya msingi sana na wala hukujali. Nilikuwa sina jinsi.

Doris : Lakini nilikuwa na matatizo makubwa.

Alex: Makubwa? Kumbuka ulikuwa unafanya kazi chini ya mkataba.

(Nyumbani kwa Batuli)

Batuli : Mbona umetutembelea usiku namna hii?

Doris : Hata sijaketi umenianza na maneno? Shikamoo dada.

Batuli : Marahaba. Kulikoni huko? Maana wewe ni maajabu kukanyaga ndani ya nyumba hii.

Doris : Kwani kuna tatizo mimi nikija kukusalimia dada?

Batuli : umekuja kutusalimia? Na Yule kiwete wako huko nyumbani umemwachia nani?

Doris : Dada, kwa nini unakuwa na maneno ya kashifa hivyo?

Batuli : Maneno gani ya kashifa? Wewe si ulijifanya umefika sana katika maisha? Nenda sasa

ukale hayo maisha yako ya raha. Nimekutafutia kazi umeichezea, sasa utajua jinsi ya

kumtunza huyo kiwete wako. Ama utaenda barabarani utajiiza? Utajijua mwenyewe?

Doris : Sawa, lakini dada kumbuka mimi ni mdogo wako na una haki ya kunisaidia bado.

Batuli : Sikiliza nikwambie wewe kikaragosi, hapa kwangu hakuna msaada kama utaendelea

kung'ang'ania huyo kiwete wako.

Doris: Kumbuka yule ni binadamu kama binadamu wengine. Ana haki ya kusaidiwa.

Batuli : Acha mawazo ya kimasikini wewe. Yule ana faida gani kwa sasa jinsi alivyo?

Doris : (Kimya)

Batuli : Utafute mtu mwingine wa kukupa misaada, lakini siyo sisi. Nafikiri umenielewa.

Doris: (Kimya)

(Nyumbani kwa Doris)

Doris : (Kwenye simu) Nilikuwa nimemwambia mume wangu kwamba sitarudi tena kazini kwa Alex kwa sababu Alex alikuwa ananitaka kimapenzi.

Batuli : Usiwe mjinga Doris. Kila mmoja anaangalia maisha yake.

Doris : (Kimya)

Doris : Daniel, naomba kujua kuna nini kinaendelea hapa. Huu ni mwisho wa mwezi sasa, ndani ya nyumba hakuna pesa ya umeme, hakuna pesa ya maji, hata pesa ya majukumu madogo imekushinda? Unategemea nini? Na wewe nakuona uko huko tu hueleweki.

Daniel : Mke wangu Doris una nini?

Doris : Hilo silo swali Daniel. Nataka kujua nini kinaendelea humu ndani. Usiniletee habari za kitoto.

Doris : Lakini mke wangu, hapa siyo suala la mimi nikijibu. Tushauriane tufanye nini.

Doris : Daniel, nimechoshwa! Nimechoshwa na hizi porojo zako za kila siku.

Daniel : Ningependa utulie tuongee kwanza tuelewane. Unajua tangu nilemae miguu, bado sijamwambia dada Rehema anayeishi London.

Doris : Hujamwambia?

Daniel : Dada Rehema wa London.

Doris : Hivi una akili timamu kwenye hiki kichwa chako? Una akili wewe? Huoni aibu? Mtu yuko London na wewe uko Tanzania, ukishamwambia atakusaidiaje?

Daniel : Tutaomba msaada, halafu tufanye lile ambalo tumekusudia.

Doris : Huoni haya? Huoni haya mwanamume mzima kuomba msaada kutoka kwa dada yako?

Daniel : Lakini kumbuka kwamba nimeshalemaa.

Doris : Kumbe unalijua hilo? Ni heri ukaombe hao vilema wenzako msaada. Pumbavu mkubwa! Kwanzia sasa, nimechoka na haya maisha, naenda zangu kutafuta kazi. Usinisumbue kwa lolote. Unanielewa?

Daniel: Doris

Doris : Wewe! Ukome! Kwanzia leo nisisikie ukitamka hilo jina.

Daniel : (Kimya)

(Jioni chumbani kwa Doris, baada ya Doris kupata kazi ofisini kwa Alex)

Daniel : Doris.

Doris : Nimelala.

Daniel : Ulipoondoka leo asubuhi, uliondoka na hasira sana. Naomba unipandishe kitandani tuongee.

Doris : Sikiliza wewe kiwete. Mbona hunielewi? Si nimekwambia nimelala? Unajua maana ya kulala au huelewi? Una matatizo gani?

Daniel : Basi nimekubali ndiyo umelala, basi naomba unipandishe kitandani nipumzike mke wangu.

Doris : Hivi nikwambie lugha gani lakini? Nimekwambia nimechoka nimelala. Kwa nini hunielewi wewe kiwete?

Daniel : Unaniumiza mke wangu.

Doris : Sijui nikupeleke wapi. Sijui nikupeleke kwa viwete wenzio. Yaani sijui nikutupe wapi mbwa wewe.

Daniel : (Kimya)

(Asubuhi chumbani kwa Doris na Daniel)

Daniel : Habari za asubuhi mke wangu?

Doris : (Kimya)

Daniel : Ulipoondoka jana ulifanikiwa kupata kazi? Kwa kweli Mungu yupo pamoja nasi.

Doris : Wewe mwanamume wewe! Uko sawa kweli? Yaani mke wako kupata kazi unashangilia? Halafu wewe unafanya nini? Umekaa tu nyumbani umestarehe.

Daniel : Lakini mke wangu Doris, kwani niliomba hali hii itokee?

Doris : Nimesema sitaki ngojera zako. Unanisikia? Na kwanzia sasa hivi, ninapokuwa kazini, simu zako zisizokuwa na maana sizihitaji. Unasikia ?

Daniel : Sawa.

(Siku inayofuata)

Daniel : Doris.

Doris : Ndiyo mume wangu kiwete. Sikiliza, natoka, nitakapokuwa kazini, simu zako zisizokuwa na maana sizihitaji. Sawa wewe kiwete ?

Daniel : (Kimya)

(Siku inayofuata)

Daniel: Doris, mbona unafanya mambo ya kipuuzi hivi?

Doris : Sikiliza wewe kiwete, mimi nimechoshwa na wewe. Usiniingilie katika maisha yangu.

Niache niendeleee na starehe zangu.

Daniel : (Anampiga Doris)

Doris : Unanipiga mimi? Shetani mkubwa wewe! Naondoka, nakuacha na huo ulemavu wako.

Daniel : Usifanye hivyo. Naomba usiodoke. Njoo tuongee mke wangu. Naomba unisamehe.

(Ofisini kwa Alex)

Rachel : Wewe kinyago, unafanya nini hapa?

Doris : Wewe mwanamke, usiniite kinyago.

Alex : Rachel, sitaki matatizo ofisini mwangu.

Rachel : Ofisi unaijua wewe. Nakupa dakika kumi utoe hii takataka hapa kama kweli hutaki fujo ofisini kwako.

Doris : Wewe mwanamke wewe! Unaniita takataka unanijua?

Rachel : Nakujua vizuri... mke wa kiwete. Tulia na kiwete wako, siyo kudadia mabwana za watu. Utaumia.

Doris : Mshenzi wewe.

Alex : Wewe mwanamke, toka nje kabla sijakuletea walinzi hapa.

Rachel : Naondoka ila kitu ambacho nitakuja kukufanyia, hutakisahau katika maisha yako.

Alex : Dua la kuku hilo, haliwezi kumpata mwewe.

Kiambatisho IV

Data ya filamu ya *Majuto*

Irine : Hebu tuwache maneno twende tukalale.

Rita : Nani alale na wewe ?

Irine : Rita, mbona wewe kila siku ni mtu wa ugomvi?

Rita : Na kwa nini wewe unapenda sana kujipendekeza kwangu? Toka nje!

Irine : Hapana, wewe ndiye utatoka nje. Unarudi saa nane usiku nakuja kukufungulia mlango unanitukana?

Rita : Nyie kunguni fungua mlango. Mbuzi nyie.

Irine : Mama unasikia matusi ya Rita?

(Asubuhi, sebuleni)

Rita : Mimi niko tayari kuondoka mama. Una jipya lolote lile?

Mama : Yaani, hata hatusalimiani?

Rita : Wewe mama, tangu nikiwa mchanga hadi nimefika hapa, bado hujachoka na hizo shikamoo?

Mama : Ni vizuri mimi kufahamu umeamkaje. Kuna kosa mama?

Rita : Mimi ninachohitaji kujua ni kuwa, kuna jipya gani? Hayo maneno ya shikamoo sina muda nayo.

Mama : Sawa. Nyumbani tumeishiwa na matumizi yamepungua sana.

Rita : Mama, leo siachi hata shilingi. Nataka huyu *house girl* wa humu ndani ajue umuhimu wangu kwake.

Mama : Sawa, *house girl* hahusiki, na mimi mama yako je?

Rita : Wewe na huyu ni kitu kimoja. Sawa nyau na paka.

Mama : (Kimya)

(Jioni ndani ya chumba cha mankuli)

Rita : Kwa hiyo wewe umeninyima mimi chakula?

Irine : Inabidi nicheke. Basi ni maajabu haya jamani. Unalalamikiaje chakula wakati umetunyima hela humu ndani?

Rita : Hiki chakula ambacho umepika ndicho unaninyima mimi? Ninaweza kununua zaidi ya hiki na huwa nawalisha kla siku humu ndani.

Irine : Hiyo kila siku , leo iko wapi? Leo ni moja katika siku ya hizo kila siku au siyo siku?

Rita : Yaani maneno yote hayo kisa wewe ndiye umenunua chakula? Kweli binadamu husahau fadhila. Kuleni basi tuone kama mtanenepa kwa siku moja.

Irine : Ulitunyima chakula ukifikiri hatutakula?

(Asubuhi, chumbani kwa Irine na Rita)

Rita : Umetoka wapi sasa hivi?

Irine : Sasa nimetoka wapi, nikujiibu wewe kama nani?

Rita : Umeanza umalaya?

Irine : Mimi nakushangaa.. unaongea na nani kwenye toni ya namna hiyo?

Rita : Naongea kama mwenye nyumba.

Irine : Unaropokea nani?

Rita : Wewe hapo.

Irine : Wewe kijibwa wewe, acha kuniropokea.

Rita : Umeanza lini kunijibu kwa namna hiyo?

Irine : Nimeanza kwanzia siku ambayo wewe ulianza kuwaona watu kwa madharau humu ndani.

Rita : Leo iwe mwanzo na mwisho kurudi nyumbani asubuhi wewe changudoa.

Irine : Kwa sauti yako nimeshituka...paka wewe.

(Asubuhi sebuleni)

Mama : Naomba nikuulize kitu kimoja. Tangu uanze ukorofi katika hii nyumba, umefaidi kitu gani? Irine ni dada yako. Kaa chini na Irine mjadiliane ili mweke kando tofauti zenu.

Rita : Sina muda mchafu wa kukaa na kinyago kama Yule na kuzungumza naye.

Mama : Mtoto niliyemzaa hawezi kuitwa kinyago. Sitaki umwite mwanangu kinyago.

Rita : Irine ni kinyago. Na wewe vilevile, unaweza ukawa kinyago.

Mama : (Kimya)

Rita : Sasa cha msingi hapa, nakupa mambo matatu umweleze huyo mwanao. La kwanza, aache kabisa umalaya. La pili, aache kabisa kiburi chake na la tatu ambalo ni la msingi kupita yote, akome kabisa kulala nje ya nyumba. Nimemaliza. Msipofanikisha haya, sitazungumza mara mbili. Kumbukeni kabisa maisha yenu yapo mikononi mwangu.

Mama : (Kimya)

(Nyumbani kwa Elvin)

Elvin : Hivi unajua wewe mwanamke kuwa nimegundua kwamba wewe ni mbishi? Kichwa chako ni kigumu sana kuelewa.

Rita : Unaniitaje mimi?

Elvin : Ndivyo hivyi nilivyokuita.

Rita : Unaniita mimi mwanamke?

Elvin : Nilikuita hapa asubuhi hii? Ulikuwa na miadi na mimi? Wewe umekurupuka huko ulikotoka umekuja huku.

Rita : Vizuri sana. Sasa basi, mimi siendi kazini wala popote pale.

Elvin : Hilo ndilo tatizo la kuishi bila mpangilio. Wewe siyo mwanamke wa kisasa. Hauko sawa kabisa.

Rita : Nina mipango mingi.

Elvin : Naomba uondoke.

Rita : Siwezi kuodoka nikuache katika hali hii.

Elvin : Ondoka ! Nahitaji kukaa peke yangu.

Rita : Mtu ambaye yuko sawa hawezi akataka kukaa pekee yake.

Elvin : Naomba uondoke!

(Usiku chumbani kwa Rita na Irine)

Rita : Makubwa leo! Kitandani mapema yote hii? Una nini mwenzetu?

Irine : (Kimya)

Rita : Tuna bubu humu ndani.

Irine : (Kimya)

(Nyumbani kwake Elvin)

Elvin : Rita, nilikwambia nini wewe?

Rita : Kuhusu nini?

Elvin : Nilikwambia usije humu ndani bila kunitarifu.

Rita : Na wewe kwani unaenda kujitambulisha bila kunitarifu?

Elvin : Nani amekwambia mambo haya?

Rita : Ninajua kila kitu kinachoendelea. Naomba utulie papo hapo. Huendi popote.

Elvin : Rita , naomba uondoke.

Rita : Siwezi kuondoka.

Elvin : Ondoka sasa hivi kabla sijakufanyia kitu kibaya.